SportPesa
TZS. 559,183,880
NI YA KWAKO WIKI HII,
BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



**Sitta** atajwa kesi uhujumu uchumi ya vigogo wa reli

UKURASA 3


ama
ALHAMISI OKTOBA 7, 2021
AFYA NA MAZINGIRA

Ukurasa 13
Usafirishaji haramu wa binadamu unavyobeba hatari ya nafsi zao

Ukurasa 12
Makuu ya binti miaka 15 asiyejiweza tangu miezi 2, vyote kwa mama mjane

MIAMBA NA MAPOROMOKO YA KIMANI …
Penye jiografia alikojificha Chifu Mkwawa pakiwapo miamba, mazingira ya kipekee

Askari mwongoza watalii, Leonard Mwakajange, akionyesha fuvu alilotumia Chifu Mkwawa, kwa ajili ya kufanyika maombi mbalimbali. PICHA: CHRISTINA HAULE.

Na Christina Haule, Mbarali

UNAPOTAJA maporomoko ya maji ya Kimani na Nyarugenge, ni kivutio na utalii wa kipekee ulio wazi kutembelewa na jamii yenye pango la Chifu Mkwawa Mkwavinyika, shujaa wa kabila la Wahehe.

Huyo anatajwa aliishi miaka 800, akijificha dhidi ya Wajerumani, kabla ya kujipiga risasi mwenyewe huko Kalenga, mkoani Iringa.

Askari Mwongoza watalii katika Pori la Akiba Mpanga Kipengere, iliyo chini ya Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA), Lenard Mwakajange, anatoa historia ya maporomoko hayo kwa waandishi wa habari, waliotembelea eneo hilo kushuhudia mambo ya kitalii mahali hapo.

Anasema umaarufu wa maporomoko hayo unatokana na kuwapo miamba mikubwa na miinuko iliyojipanga kama ngazi, kupendezesha maporomoko hayo.

Mwakajange anasema, Chifu Mkwawa aliishi katika pango la asili kuanzia mwaka 1891 hadi 1898, mahali kando na maporomoko ambayo ametumia maji yake kuoga, pia kufua vyuma kutokana na kuwapo kiwanda kidogo cha kutengeneza silaha za jadi na za kivita, ili kukabiliana na wapinzani wake.

Mwakajange anasema, kwenye maporomoko hayo ya Kimani na Nyarugenge, kumekuwa kivutio cha pango lililotumiwa na Chifu Mkwawa na ukambebesha umaarufu mkubwa, kutokana na kuwapo harufu ya mimea mbalimbali inayowavutia watalii wa ndani na nje ya nchi.

Anashauri, wananchi wazuru mahali hapo na kukagua mahali ambako pango la Chifu Mkwawa lilipo, tofauti na mengine kutokana na kuwa na umbo la bati, hata kuwezesha mvua za masika zinavyotiririka kwa wingi yanapita juu ya pango na kumwagika mbele ya pango, sehemu kubwa inagubikwa na maji.

Mwongoza watalii huyo anasema, hali ya maji kupita juu ya pango imechangia maisha ya Chifu Mkwawa kubaki salama na ndiyo imekuwa namna bora ya kificho hata hakukamatwa na Wajerumani waliomsaka.

Askari huyo anasema, katika eneo hilo la pango kuna fuvu la kichwa cha nyani, ambalo Chifu Mkwawa alilitumia kwa matambiko mbalimbali na kwa sasa jamii za makabila ya Wahehe, Wabena, Wakinga na Wahanji nao wamekuwa wakifika kuzuru na kufanya matambiko yao.

Mtaaluma huyo wa hifadhini, anapasifu kuwa mahali palipojaa utajiri wa maporomoko yenye maji mengi nyakati zote na miamba mikubwa, inayovutia.

Anapafafanua kwamba ni mahali ambako kumezungukwa na viumbe ndege na nyani wanaoogelea katika makundi ya koo tatu tofauti, huku kukiwapo mvuke mkubwa unaotokana na maji yanayopita kutoka kilele cha juu cha kwenye maporomoko hayo.

"Maporomoko ya maji ya Kimani yana takribani mita mia na hamsini na mabwawa mbalimbali yanayoleta ladha ya watu kuja kutembelea, kurekodi video mbalimbali, kuogelea, kujifunza miamba kwa wanafunzi," anasimulia.

Anaendelea kuhusu kinachovutia watu ni: "kuona wanyamapori kama nyani wa njano 'yellow baboon', ndege aina tofauti na ni eneo linaloruhusu makazi ya wanyama kama Tandala na Ngorombo."

Mhifadhi Mwandamizi wa Pori la Akiba la Mpanga Kipengere, Alfred Kipondamali, anaeleza pori hilo lina zaidi ya maporomoko saba ya maji, yaliyoko katika maeneo tofauti maarufu na kwa sasa yalioendelezwa na kutumika kwa utalii ni Kimani na Nyarugenge.

"Hili pango ni sehemu maarufu sana kwa utalii na watu wamekuwa wakifika hapo. Tumelitunza, kwani ni pango zuri la kutalii na kuonyesha na historia katika nchi yetu,"aanasema.

Pango la Chifu Mkwawa, lilianza kutumika kama maficho wakati wa vita vya Wajerumani na Wahehe kati ya miaka ya 1855 hadi 1898 na kwamba pango pamoja na maporomoko hayo, yanapatikana katika eneo la Mbarali, jirani na barabara kuu ya Dar es Salaam - Mbeya

UKURASA 11

Alhamisi Oktoba 7, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0580726
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Kesi za talaka zazidi kutikisa

## **Dar** yaongoza, Samia abaini shida haki Mahakama za Mwanzo

*Endelea ukurasa 2*



Rais Samia Suluhu Hassan, akifungua pazia kuzindua jengo la Kituo Jumuishi cha Utoaji Haki, jijini Dodoma jana. Watatu kulia ni Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Juma, Jaji Mkuu wa Zanzibar, Othman Makungu (wapili kulia), Waziri wa Sheria na Katiba, Prof. Palamagamba Kabudi (wapili kushoto) na Spika wa Bunge, Job Ndugai (kushoto). **PICHA: IKULU**



UKURASA 3

# Assad: Sikumaliza muda nafasi CAG

UKURASA WA 4

### MAREKANI YASAIDIA KUAJIRI WATAALAMU 100 SEKTA YA AFYA

SERIKALI ya Marekani, kupitia mradi wa Afya Endelevu wa Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID), imesaidia kuajiri wataalamu wa afya...

UKURASA WA 8

### SERIKALI YAFUTA MAPORI 12, WANANCHI KUNUFAIKA

SERIKALI imefuta mapori 12 yenye ukubwa wa ekari 707, 659 na misitu 12 ya ukubwa wa ekari 46,755, kwa ajili ya kuwapatia wananchi, kuendesha shughuli...

# Waliochanja Corona wafikia 680,000

UKURASA 4



UKURASA WA 8

### MBARAWA AINYOOSHEA KIDOLE TRC MAPATO

WAZIRI wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, amelitaka Shirika la Reli Tanzania (TRC) kusimamia ukusanyaji...

UKURASA WA 9

### NAIBU WAZIRI ATAKA KUIMARISHWA KAMATI ZA ULINZI WA MAMA, MTOTO

NAIBU Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mwanaidi Ali Khamis, ameagiza kuimarishwa kwa kamati za ulinzi na usalama...



MICHEZO STARS YAAHIDI KUIMALIZA BENIN UK.24
MAONI, KATUNI UK.6




Muhubiri wa Kimataifa na Mkuu wa Taasisi ya Christ for All Nations (CfaN), Daniel Kolenda (kulia), akizungumza na waandishi wa habari jana, baada ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla (katikati), kuzindua mikutano mikubwa sita ya injili itakayofanyika katika sehemu sita za Jiji hilo za Kawe, Jangwani, Kimara, Mbagala, Gongo la Mboto na Kigamboni, yenye kauli mbiu ya Imani, Upendo, Miujiza. Kushoto ni Askofu wa Kanisa la CPCT, Sylvester Gamanywa. **PICHA: JOHN BADI**

# Kesi za talaka zazidi kutikisa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MKOA wa Dar es Salaam umetajwa kuongoza kuwa na idadi kubwa ya mashauri ya mirathi, ndoa na talaka nchini.

Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Juma, alibainisha hayo kwenye uzinduzi wa kituo jumuishi cha utoaji haki jijini Dodoma, ambacho ni miongoni mwa vituo sita vilivyojengwa kwenye mikoa ya Arusha, Mwanza, Dar es Salaam na Morogoro kwa mkopo kutoka Benki ya Dunia (wb) kupitia mradi wa maboresho ya mahakama.

Alisema uamuzi wa kujenga mahakama jumuishi Temeke ulisukumwa na uwapo wa idadi kubwa ya mashauri ya mirathi, ndoa na talaka mkoani Dar es Salaam.

"Kwa mfano, kati ya mwaka 2017 hadi 2019 kulikuwa na mashauri 7,600 ya mirathi ambapo kati yake 3,765 yalikuwa katika ngazi za mahakama za mwanzo. Mashauri ya ndoa na talaka yalikuwa takribani 4,200 kati ya mwaka 2017 na 2019," alibainisha.

Vilevile, alisema uhitaji wa kuwa na mahakama maalum Temeke ni muhimu kutokana na mapendekezo ya wadau wa mahakama ambao wamekuwa wakijenga hoja ya kuwa na mahakama hiyo ambayo itashughulikia mashauri ya kifamilia.

Akifafanua zaidi kuhusu mirathi, Prof. Juma alisema ni eneo ambalo lina ucheleweshwaji mkubwa na lina malalamiko mengi.

"Kumekuwa na ulegevu kwa upande wetu wa mahakama wa kuwadhibiti wasimamizi wa mirathi ili wafunge mirathi, na eneo ambalo kuna changamoto ambapo mara nyingi wasimamizi wa mirathi hujigeuza kwamba wao ndio warithi na mara nyingi wanaoumia zaidi ni wajane na watoto," alisema.

Kutokana na hali hiyo, Jaji Mkuu alisema waliona umuhimu wa kuwa na mahakama ambayo itasaidia kujua hali halisi ya matatizo na masomo watakayoyapata kwenye mahakama hiyo, yatasaidia kuboresha utoaji haki kwa kundi hilo ambalo lipo mbali na fursa ya upatikanaji haki.

Aliwataka watumishi waliopangwa kwenye kituo hicho kutambua dhamana waliyo nayo kutokana na kuwa ni kituo cha mfano kushughulikia mashauri hayo.

"Watumishi watambue kwenye Kituo cha Temeke wanandoa na wanafamilia huwa wanatoa matatizo yao ya siri sana ambayo hayatakiwi kutoka, yanatakiwa kuishia pale na mara nyingi wanahitaji huduma za saikolojia na huduma ya usuluhishi, msijikite kuangalia sheria, mjikite kwa yale yanayozunguka sheria," aliagiza.

Awali, alitaja sababu ya kujenga vituo vya Temeke na Kinondoni kwenye mkoa huo kuwa ni kutokana na wingi wa mashauri ambapo kwa Mahakama Kuu ya Kanda ya Dar es Salaam kwa takwimu za Septemba mwaka huu, kulikuwa na mashauri zaidi ya 3,000.

"Idadi ya watu Dar es Salaam imeongezeka sana na mahitaji ya mahakama yameongezeka sana na hiyo ndio sababu ya kuwa na mahakama jumuishi Temeke na Kinondoni," alisema.

**HALI HALISI KITAIFA**

Takwimu za Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA) za mwaka jana (2020) zinaonyesha wakala ulisajili talaka 511 Tanzania nzima. Kati yake, 221 zilitoka Dar es Salaam pekee. Idadi hiyo ni ongezeko la talaka 69 kulinganishwa na talaka 442 zilizosajiliwa mwaka 2019.

Msajili wa Ndoa na Talaka wa RITA, Jane Barongo, alikaririwa Januari mwaka huu, akibainisha kuwa Dar es Salaam inaongoza kwa talaka zinazowasilishwa na wanandoa wenyewe.

"Huwa tunapokea maombi ya kusajili talaka kutoka mahakamani na wateja binafsi, Dar inaongoza kwa watu binafsi kuleta wenyewe maombi kutaka kusajili vyeti vya talaka," alibainisha Jane.

Mwezi uliopita, Nipashe ilizungumza na Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi Inayoshughulika na Masuala ya Ndoa, Familia na Malezi Tanzania (TaMCare), Dk. Enock Mlyuka, anbaye alisisitiza kuwa ndoa ni kitovu cha familia na malezi, lakini vijana wengi siku hizi wanakimbilia kuingia kwenye uhusiano bila kuzingatia msingi halisi wa ndoa.

Dk. Mlyuka ambaye ni Mchungaji wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), alianika uzoefu wake, akisema: "Haipiti siku sijapata simu au mtu amekuja ana mgogoro na mwenza wake."

Kurejea katika hafla ya jana jijini Dodoma, Waziri wa Katiba na Sheria, Prof. Palamagamba Kabudi, alisema ufunguzi wa kituo hicho unafanyika wakati taifa linajiandaa kusherehekea miaka 60 ya uhuru wake likiwa limepiga hatua kubwa ya kimaendeleo.

"Nithubutu kusema katika miaka 60 ya uhuru ambayo Rais wetu Samia ni sehemu ya historia hiyo, nchi imepiga hatua kubwa.

"Wakati tunapata uhuru mwaka 1961, mahakama hii haikuwa jumuishi, lakini leo tunazungumza kituo jumuishi, kipindi hicho wenyeji ambao ni Waafrika, hawakuwa na mfumo wa mahakama. Mahakama ilikuwa kwa ajili ya wazungu na wahindi, waafrika walihukumiwa na machifu, rufani ilienda kwa mkuu wa wilaya, kwa mkuu wa mkoa na kwa gavana na hapo ndio ilikuwa mwisho," alisema.

Mtendaji Mkuu wa Mahakama, Prof. Elisante Ole Gabriel, alisema kuna mahakama za mwanzo 960 huku upungufu ukiwa mahakama 2,996 na kwa ngazi ya wilaya, mahakama zilizopo ni 139 na upungufu ni 20.

Alibainisha kuwa kwa Tanzania Bara, kuna watumishi 5,835 ilhali mahitaji ni watumishi 10,350.

## Samia abaini shida utoaji wa haki mahakama za mwanzo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan, amebaini kuwapo na shida kwenye uamuzi wa Mahakama za Mwanzo na kutaka kuangaliwa kwa jicho la kipekee.

Samia aliyasema hayo jana kwenye uzinduzi wa Kituo Jumuishi cha utoaji haki jijini hapa ambavyo ni miongoni mwa vituo sita vilivyojengwa kwenye mikoa ya Arusha, Mwanza, Dar es Salaam na Morogoro kwa mkopo kutoka Benki ya Dunia kupitia mradi wa maboresho ya mahakama. Alitaka kuwapo na usimamizi wa ubora wa uamuzi kwenye mahakama hizo kwa kuwa malalamiko mengi yanazihusu.

Rais Samia alihimiza usikilizaji wa kesi kwa haraka na watoaji haki wasikubali kirahisi kubadili mahakimu au tarehe za kusikiliza kesi kwa kuwa ni miongoni mwa sababu za ucheleweshaji.

Alisema pamoja na ujenzi wa miundombinu ya utoaji haki, haitawezekana kupata mafanikio yanayotarajiwa endapo wasimamizi na wadau wa mfumo wa utoaji haki hiyo hawatafanya kazi kwa kuzingatia sheria, taratibu na kuongozwa na nafsi.

"Ina maana kwamba tunaweza kuwa na majengo mazuri sana yenye kila huduma, mfumo mzuri wa TEHAMA na kila kitu tunachokihitaji, kama watendaji, mahakimu, majaji na wengine wanaowasaidia hawakuongozwa na nafsi njema katika utoaji haki bado haki inaweza isipatikane, inaweza kutumika kugeuza haki, mwenye haki akanyimwa na asiye na haki akapewa," alisema.

Aliwataka watoaji haki kwa wananchi kuhakikisha inatolewa vile inavyopaswa na kushughulikia suala la ucheleweshaji wa kesi.

"Pamoja na rai napongeza pia huu mfumo wa TEHAMA unaotumika unampa Jaji Kiongozi kujua kesi gani imekaa kwa muda gani haijasikilizwa na kumuuliza Jaji aliyepewa kesi sababu ya kutosikilizwa, hii itashtua mahakama na itashtua wale wengine wanaowachelewesha wapelelezi, mawakili, polisi na magereza na wenyewe watapata msukumo," alisema.

Alibainisha kuwa uwapo wa vituo hivyo jumuishi utapunguza ucheleweshaji wa kesi na gharama kwa wananchi. "Changamoto kubwa inayokabili mfumo wa utoaji haki ni ucheleweshaji wa kesi, hivyo uanzishaji wa vituo hivi jumuishi utapunguza tatizo hilo la ucheleweshaji wa kesi," alisema.

Aliahidi serikali kuendelea kuiwezesha mahakama katika kutekeleza majukumu yake ikiwamo kukamilisha ujenzi wa Makao Makuu ya Mahakama yanayojengwa Dodoma.

Kadhalika, kuhusu kituo cha Temeke kushughulikia mashauri ya kifamilia, Rais Samia alisema suala hilo ni kubwa kwa kuwa wanawake wengi na watoto wamekuwa wakiteseka kwenye mambo hayo na inatokana na kutowajibika kwa wanaume.

"Hili ni funzo kwa wanaume wawajibike, umeacha mtoto mahali wajibika usijifiche huyo ni kiumbe alikuja bila kutaka mwenyewe ulimleta nenda kawajibike, shirikiana na uliyeshirikiana naye kumleta duniani," alisema.

Alisema kuwa kituo hicho kitasaidia kuondokana na mrundikano wa kesi za aina hiyo na kitatoa mafunzo ya kushughulikia migogoro ya mirathi na matunzo nchini.

Alisema mikoa tisa bado haina Mahakama Kuu na kujitaja kuwa ni Njombe, Geita, Singida, Manyara, Pwani, Katavi, Songwe, Lindi na Simiyu na kuitaka Mahakama kwenye mpango mkakati wa miaka mitano ijayo kuipa kipaumbele.

"Tumeanza kufanya majaribio ya mahakama za kutembea kwenye Mikoa ya Dar es Salaam na Mwanza ambapo tunatarajia kuzitanua kwenye awamu ya pili ya mradi wa maboresho ya huduma za utoaji wa haki, tunaelewa bado hakuna idadi ya kutosha ya watumishi tutaendelea kuongeza ili haki zipatikane kwa wakati," alisema.

## HABARI KITAIFA



Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Shinyanga, Lucy Mayenga (kushoto), akikabidhi taulo za kike kwa Mwalimu Mkuu wa Shule ya Sekondari Mwendakulima, Neema Daniel, shuleni hapo jana, kwa ajili ya wanafunzi wasichana ili ziwasaidie kuhudhuria masomo pindi wanapoingia kwenye siku zao. Mbunge huyo pia alikabidhi kompyuta tano na printa moja zenye thamani ya Sh. milioni 10. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Sitta atajwa kesi uhujumu kigogo wa reli

**Na Kulwa Mzee**

MCHUNGUZI Mkuu kutoka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Malimi Mifuko, amedai kuwa aliyekuwa Waziri wa Uchukuzi, Samuel Sitta, alikuwa akiufahamu mchakato wa zabuni ya ujenzi wa reli ya kisasa.

Sambamba na kuufahamu mchakato huo, amedai kuwa Sitta (sasa marehemu), alitoa maelekezo kwa aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni Hodhi ya Rasilimali za Reli (RAHCO), Benhardard Tito.

Mifuko ni shahidi wa saba katika kesi ya uhujumu uchumi inayomkabili Tito na wenzake wanaotuhumiwa kwa matumizi mabaya ya madaraka.

Akiongozwa na Wakili wa Serikali, Maghela Ndimbo, mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Joseph Luambano, shahidi huyo alidai walipokea malalamiko na kwamba yanapokuwepo lazima uchunguzi ufanyike.

Alidai kuwa walikusanya nyaraka ili kujiridhisha kama zabuni ya ujenzi wa reli ya kisasa ipo na katika uchunguzi walibaini zabuni ipo na mchakato ulishaanza.

Hata hivyo, shahidi huyo alidai kuwa kulikuwa na ukiukwaji wa taratibu za ununuzi na hicho ni kiashiria tosha cha kuwapo kwa tatizo kwenye mchakato mzima wa zabuni.

Alidai alikusanya nyaraka kutoka sehemu mbalimbali kwa ajili ya ukaguzi ikiwemo RAHCO kwa Mkaguzi wa Fedha, Mkaguzi wa Ndani, Benki ya CRDB na miongoni mwa nyaraka hizo ilikuwa nakala za mkataba wa ujenzi wa reli.

Shahidi anadai hawakupata mkataba halisi katika maeneo yote waliyoelekezwa na mshtakiwa wa kwanza, Tito.

Alidai nyaraka mojawapo ilikuwa ya CRDB ya kuomba kufungua akaunti ya malipo ya Dola za Marekani 500,000 kwa Kampuni ya Rothschild ya Afrika Kusini na kulikuwa na maombi mengine ya malipo ya Dola milioni 100 kwa Kampuni hiyo ya Rothschild.

Mchunguzi huyo alidai kuwa alikwenda kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambako RAHCO ilipeleka mkataba kwa ajili ya uhakiki na uhakiki ulipofanyika ilibainika kuna marekebisho katika mkataba ili ukidhi matakwa ya kisheria.

Ilidaiwa kuwa mwanasheria mkuu alitoa maelekezo ya kufanya marekebisho katika mkataba Mei 22, 2015 lakini maelekezo hayo hayakutekelezwa kwa kuwa mkataba ulikuwa umeshatiwa saini Mei 20, mwaka huo.

Shahidi alidai kuwa alifika Wizara ya Uchukuzi na aliwasiliana na Sitta wakati wa uchunguzi. "Mheshimiwa Samweli Sitta alisema anaifahamu hiyo zabuni, alielewa mchakato upo na alitoa maelekezo mbalimbali.

"Alimwandikia barua Mkurugenzi wa RAHCO (mshtakiwa wa kwanza, Tito) akimwelekeza aiarifu Kampuni ya Rothschild kuwasilisha dodoso na alielekeza utekelezaji uende kwa kasi," alidai.

Anadai katika uchunguzi ilibainika kwamba kampuni hiyo ya Afrika Kusini, ililipwa Dola za Marekani 500,000 bila kufanya kazi yoyote.

"Katika zabuni, sheria ya ununuzi wa umma haukufatwa, taratibu za kutangaza zabuni hazikufanyika. Nyaraka za upembuzi yakinifu zilikuwa hazijakamilika na fedha zililipwa, hivyo kusababisha RAHCO kupata hasara ya Dola za Marekani 527,540. Upembuzi yakinifu ungefanyika ungesaidia kujua gharama ya mradi, ungewezesha kupata fedha na mambo mengine ikiwamo kuonyesha athari za mazingira.

"Mkurugenzi wa Fedha wa RAHCO alithibitisha malipo yalifanyika kwa mtu ambaye hakufanya kazi. Mshtakiwa Tito alikuwa mtendaji mkuu na alipaswa kuhusisha bodi ya zabuni, kufuata utaratibu wa ununuzi wa umma na hakupaswa kusaini (kutia saini) mkataba kabla maelekezo ya mwanasheria mkuu wa serikali hayajatekelezwa,"alidai Mifuko.

Mifuko alidai mshtakiwa Emmanuel Massawe alipaswa kumshauri mtendaji mkuu katika masuala ya zabuni na mshtakiwa Kanji Mwinyijuma alihusika kupokea nyaraka kwa niaba ya Kampuni ya Rochschild na alitia saini kwa niaba wakati hakutumwa kufanya hivyo.

Washtakiwa katika kesi hiyo wanakabiliwa na mashtaka manane ikiwamo matumizi mabaya ya madaraka wakati wa mchakato wa kumpata mshauri mwelekezi katika ujenzi wa reli ya kisasa.

Mbali na Tito, washtakiwa wengine ni Mwanasheria wa RAHCO, Emmanuel Massawe na mfanyabiashara ambaye pia ni mwakilishi wa Kampuni ya Rothschild (South Africa) Proprietary Limited, Kanji Mwinyijuma.

Katika kesi ya msingi, washtakiwa hao wanakabiliwa na mashtaka yakiwamo ya uhujumu uchumi, matumizi mabaya ya madaraka, kula njama na kuisababishia RAHCO hasara ya Dola za Marekani 527,540.

Wanadaiwa kuwa kati ya Septemba Mosi na 30, 2015 kwa nia ya kutenda kosa, walikula njama kinyume cha sheria ya kuzuia na kupambana na rushwa.

Inadaiwa Februari 27, 2015 katika ofisi za RAHACO zilizoko Ilala, Tito alitumia madaraka yake vibaya kwa kuiajiri Kampuni ya Rothschild (South Africa) Proprietary Ltd kama mshauri wa mradi wa uimarishaji reli ya kati bila idhini ya Bodi ya Zabuni ya RAHCO.

Tito na Massawe wanadaiwa Machi 12, 2015 katika ofisi za RAHACO, wakiwa katika nyadhifa zao, walitia saini barua ya kuihalalisha kampuni hiyo ya Afrika Kusini kuwa mshauri wa mradi wa uimarishaji reli ya kati na kutoa huduma za ushauri wa kifedha kuhusu mradi huo.

Katika shtaka lingine, ilidaiwa kuwa Tito na Massawe, Machi 12 na Mei 20, 2015 wilayani Ilala walishindwa kuwasilisha mkataba wa huduma ya ushauri kati ya kampuni hiyo ya Afrika Kusini na RAHCO.

Tito na Massawe wanadaiwa Mei 20, 2015 katika ofisi za RAHCO, kwa kutumia madaraka yao, walitia saini mkataba wa kutoa huduma za ushauri na kampuni ya Afrika Kusini bila ridhaa ya Bodi ya Zabuni ya RAHCO.

Washtakiwa hao, wanadaiwa kati ya Mei 20 na Juni 20, 2015 walitumia madaraka yao vibaya kwa kushindwa kuwasilisha mkataba walioingia na kampuni ya Afrika Kusini kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Washtakiwa wanatetewa na Peter Kibatala na Nashon Nkungu.

# Assad: Sikumaliza muda wangu ofisini

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

ALIYEKUWA Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Prof. Mussa Assad, amesema amekuwa akikerwa na kitendo cha kuitwa 'CAG aliyemaliza muda wake' wakati ukweli ni kwamba hakumaliza muda wake, bali mchakato wa kumwondoa ulivunjwa katika nchi.

Prof. Assad alibainisha hayo jana jijini Dodoma alipozungumza kwenye mdahalo uliondaliwa na Kituo cha cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) kuhusu kitabu cha Rai ya Jenerali juzu ya tatu.

Prof. Assad alisema kuondolewa kwake madarakani kama CAG kulikiukwa kwa kiasi kikubwa misingi ya Katiba ya nchi ya mwaka 1977.

"Neno hili la kuitwa CAG aliyemaliza muda wake huwa linanikera sana! Mimi sikumaliza muda, leo (jana) hii ndiyo ninafikisha miaka 60, lakini kwa mujibu wa Katiba, CAG anapaswa kustaafu baada ya kufikisha miaka 65," alilalama.

Prof. Assad alisema kuwa kwa mujibu wa Katiba ibara ya 144, CAG anaweza kuondolewa katika nafasi yake kwanza kama ameshindwa kutekeleza majukumu yake kwa sababu ya ugonjwa au kwa sababu yoyote ile.

"Mbili, awe amefanya utovu wa nidhamu, tatu awe amevunja au kwenda kinyume cha 'Code of Ethics' kwa sababu hizi tatu tu na hilo la mwisho la kuvunja code of ethics, kama Rais anadhani suala la kumwondoa CAG madarakani ni jambo zuri, ipo 'procedure' (hatua) ya kufuata ambayo ni kuteua tume yenye watu watatu wenye hadhi ya ujaji na mmoja wapo lazima atoke Jumuiya ya Madola," alikumbusha Prof. Assad.

"Hivyo, siku ya leo (jana) kama Mungu akipenda hayo ndiyo mambo ambayo tunatakiwa kuyajadili na kuyaweka sawa," alisema Prof. Assad.

Aliongeza kuwa hivi sasa kumekuwa na viongozi ambao wameshindwa kuwajibika ipasavyo kwa sababu ya kile alichokiita kutumia magari ya kifahari au nyumba ya serikali, hivyo wanakuwa waoga kuhofia wakitolewa, watayakosa maisha ya aina hiyo.

"Tusiwe waoga, riziki siyo serikalini tu. Mbona mimi huu ni mwaka wa pili nipo mtaani na 'alhamdulai' mambo yanakwenda vizuri kabisa?" Prof. Assad alihoji.

Akijibu swali kuhusu sababu za kutokwenda mahakamani kama aliona mchakato wa kuondolewa katika nafasi yake haukufuata Katiba, Prof. Assad alisema:

"Niliongea na wanasheria wa masuala ya katiba nchini Kenya, lakini maprofesa wa hapa nchini lakini kabla sijafanya kitu, wale wa Kenya walinipigia na kunishauri kuwa wao wameona kulingana na hali ilivyo nchini kwangu, kesi hii sitakuwa na uwezo wa kushindana na serikali yangu, hivyo niachane nayo na nikihitaji msaada wowote basi niwasiliane nao," Prof. Assad alisema.


chemicotex
the brands for you

TAARIFA KWA UMMA



216496401

VENANCE URIO

Hii ni kutaarifu umma kwamba wenye picha hapo juu **Venence Urio** si mfanyakazi tena wa Chemi & Cotex Industries LTD Tawi la Musoma kuanzia tarehe 19-08-2021.

Tunaomba kuutangazia Umma kwamba kampuni ya Chemi & Cotex haitahusika na miamala itakayoingizwa au shughuli yoyote itajayofanywa na mtajwa hapo juu kwa jina la kampuni.

Utawala

# Waliochanjwa corona wafikia 680,000 nchini

**Na Maulid Mmbaga**

SERIKALI imesema hadi kufikia Oktoba 5 mwaka huu, jumla ya watu 681,736 wamepatiwa chanjo ya UVIKO-19, sawa na asilimia 66 ya dozi zilizosambazwa nchini.

Taarifa iliyotolewa jana na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, ilibainisha kuwa serikali kupitia kamati zake kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, inaendelea kuhakikisha elimu ya namna ya kujikinga na utoaji wa chanjo dhidi ya ugonjwa huo inaendelea kutolewa kwa wananchi.

Waziri huyo alisema kuanza kwa kampeni ya jamii shirikishi na harakishi nchini kumesaidia kuongeza hamasa na mwitikio wa wananchi kupata chanjo, ambapo idadi ya wanaochanja sasa imepanda zaidi ya mara 10.

"Mafanikio haya ya kampeni yanatokana na kuongezeka kasi ya uelimishaji wa wadau katika sekta mbalimbali ikiwamo Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari na idara yake ya Habari na Maelezo, wasanii wa sanaa zote, makundi mbalimbali ya kijamii yakiwamo ya vijana, wanawake, wazee, wanamichezo, vyombo vya dini na madhehebu mbalimbali na wanasiasa," alisema.

Dk. Dorothy aliongeza kuwa suala la kuhamasisha wananchi kwa kwenda nyumba hadi nyumba limesaidia kuongeza kasi ya utoaji chanjo, huku vituo vya kutolea huduma hiyo vikiongezeka kutoka 550 hadi kufikia 6,784 vinavyotoa chanjo nchini.

Waziri huyo pia alibainisha kuwa Oktoba 4 mwaka huu, serikali ilipokea shehena ya chanjo za Sinopharm na kwamba inatarajia kupokea shehena ya pili kesho na kufanya jumla ya chanjo zote zilizopokewa kuwa 1,065,000.

Alisema baada ya taratibu za uhakiki kukamilika, usambazaji utaanza na zitawafikia wananchi katika vituo vyote ambavyo kwa sasa vinatoa huduma ya chanjo huku elimu ikiendelea kutolewa na upokeaji chanjo utaendelea kuwa wa hiari kama ilivyoelekezwa na Rais Samia Suluh Hassan.

Waziri Dorothy alisema kwa sababu ya uelimishaji na mwitikio mkubwa wa wananchi kupata chanjo, baadhi ya mikoa imemaliza mgawo wa chanjo za awali na imekuwa ikiomba mikoa ya jirani, huku akiwahakikishia wizara itatoa chanjo zote mapema ili kazi iendelee.

"Nitoe wito kwa wananchi kuendelea kujitokeza kwa wingi kupata chanjo katika maeneo yao kwani chanjo hizo ni salama, zina ufanisi na ubora unaotakiwa na matokeo ya uchanjaji tumeanza kuyaona kupitia hospitali zetu kwani wanaolazwa na vifo vitokanavyo na UVIKO-19 si tatizo kwa waliochanja ukilinganisha na wale ambao hawajapata chanjo," alisema.

Licha ya mafanikio hayo, waziri huyo alitoa wito kwa wananchi kuendeleza tabia ya unawaji mikono kwa maji safi, tiririka na sabuni mara kwa mara au utumiaji wa vipukusi, uvaaji barakoa katika maeneo hatarishi, kukaa umbali wa mita moja kati ya mtu na mtu, lishe bora, kufanya mazoezi na kutumia fursa ya kupata chanjo ili kuondoa tatizo la ugonjwa huo.

"Niwapongeze sana viongozi wa mikoa na watoa huduma wote wanaoendelea kufanya kazi kwa nguvu zao zote na niwahakikishie kuwa serikali inawaona na inatambua mchango wao, naomba tusichoke, tusikate tamaa mpaka tutakapofikia lengo letu la kuwakinga angalau asilimia 60 ya wananchi wetu ili kuudhibiti kabisa ugonjwa huu, pia tuendelee kuwaepuka wapotoshaji na baadhi ya taarifa hususani kwenye mitandao ya kijamii," alihitimisha.



Mkurugenzi Mtendaji na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya Afrika (BOA), Adamu Mihayo (kulia), akizungumza na timu ya watendaji wa kampuni ya Garda World Company Ltd, wakiongozwa na Mkurugenzi Mkuu, Goodluck Lukumay (wa pili kushoto), katika kuadhimisha wiki ya huduma wateja, jijini Dar es Salaam jana. Wengine ni maofisa waandamizi wa kampuni hiyo, Mark Hart (katikati) na Fortunata Bingi (wa pili kulia) na Ephrem August. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Marekani yasaidia kuajiri wataalamu 100 sekta ya afya

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Marekani, kupitia mradi wa Afya Endelevu wa Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID), imesaidia kuajiri wataalamu wa afya 100 kushughulikia mahitaji ya dharura ya Uviko-19. Wataalamu hao watafanya kazi katika maeneo manne ambayo ni bandari na vituo vya afya 33 kwa kutoa huduma za kinga ya UVIKO-19, matibabu na kuharakisha utoaji wa chanjo Unguja na Pemba.

Taarifa iliyotolewa na Ubalozi wa Marekani jana, ilisema wataalamu hao wametambuliwa kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na wamepangwa kwenye vituo vilivyo na upungufu mkubwa wa rasilimali watu na maeneo ya kuingilia ya bandari yenye hatari za maambukizi.

Taarifa hiyo ilisema vituo vya afya nchini Tanzania vimekuwa na wafanyakazi wachache, kitu ambacho kinaathiri ubora wa utoaji wa huduma za afya.

Wakati janga la UVIKO-19 lilipoikumba Tanzania, upungufu wa wafanyakazi wa afya ulidhihirika zaidi hasa wa kusaidia huduma za kinga na matibabu ya corona. Kwa mujibu wa Ripoti ya Hali ya Serikali ya Septemba 27, 2021, matumizi ya chanjo ya UVIKO-19, yatapunguza magonjwa na vifo vinavyohusiana na UVIKO, lakini kiwango cha utoaji wa chanjo bado ni kidogo.

"Serikali ya Marekani kwa kushirikiana na Serikali ya Tanzania na Zanzibar zinapunguza athari za janga hilo kwa jamii. Mradi huu unalenga kusaidia upatikanaji na utoaji wa chanjo ya UVIKO-19, kupunguza magonjwa na vifo vitokanavyo na ugonjwa huo, kuzuia na kupunguza athari zake kwenye dharura ya VVU/UKIMWI," ilisema taarifa hiyo.

Mpaka sasa, USAID imewekeza kiasi cha Dola za Marekani million 25.1 kwenye maeneo hayo.

"Ni Muhimu kutambua kwamba Serikali ya Marekani na Wizara ya Afya ya Zanzibar zimeshirikiana kuimarisha uwezo wa wahudumu wa afya na kujenga uelewa katika kuainisha vipaumbele vya afya ya jamii mfano UVIKO-19. Kwa takribani miaka ishirini sasa, USAID imekuwa mstari wa mbele kuendeleza rasilimali watu, kwenye sekta ya afya," ilisisitiza taarifa hiyo.

Ukitekelezwa kupitia Taasisi ya Benjamin William Mkapa (BMF), mradi wa USAID Afya Endelevu unaimarisha rasilimali watu kwenye afya, eneo ambalo lina rasilimali hafifu nchini Tanzania. Kupitia Afya Endelevu, wataalamu wa afya wameelekezwa kufanya kazi na vituo vya afya teule vinavyokabiliwa na uhaba mkubwa na wameajiriwa katika mchakato wa ushindani, ambao unaangalia ustadi na sifa zinazohitajika kukabiliana na changamoto zinazojitokeza za kiafya, kama vile kuonesha mfano katika upataji wa chanjo ya UVIKO-19 na kuboresha ubora wa huduma za kinga na matibabu.

Akizungumza katika hafla hio leo, Mkurugenzi wa Afya wa USAID, Ananthy Thambinayagam alisema; "Nguvu kazi na vifaa vya kutosha ni muhimu kwa maendeleo endelevu na utoaji endelevu wa huduma bora za afya na mwitikio wa dharura kama UVIKO-19."

Alisema USAID inasaidia uwekezaji katika wafanyakazi wa afya kwa sababu nguvu kazi yenye uwezo inaokoa maisha, haswa sasa katika janga la UVIKO-19". Ananthy alisisitiza juu ya ufadhili wa USAID kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tunapoendelea kushirikiana na kudumisha mabadiliko yenye ufanisi zaidi kuelekea kwenye kutoa huduma bora za afya, ambazo zinawanufaisha Watanzania wote.

# Mwinyi akunwa kasi kutatua kero Muungano

**Na Mwandishi Wetu, Zanzibar**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, ameelezea kufurahishwa na kasi ya utatuzi wa kero za Muungano inayoonyeshwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo na mwenzake wa Zanzibar, Waziri katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Dk. Khalid Salum Mohamed.

Aliyasema hayo jana kwenye mkutano baina yake na viongozi wakati wa ziara maalumu ya kikazi iliyofanywa na Waziri Jafo, Ikulu mjini Zanzibari.

Mazungumzo hayo yalijikita kwenye mafanikio yaliyopatikana ndani ya kipindi kifupi kwa kushughulikia hoja 11 za Muungano pamoja na kazi kubwa inayoendelea ya kumalizia hoja saba zilizobaki. Akizungumza kwenye kikao hicho, Dk. Mwinyi alimpongeza Waziri Jafo na Dk. Khalid kwa ushirikiano wao mkubwa na kuchapa kazi kwa kasi hadi kuwezesha kuondoa hoja 11 kati ya 18 zilizokuwa bado hazijapata ufumbuzi awali.

Dk. Mwinyi alipongeza pia juhudi kubwa zinazofanywa kwa upande wa mazingira na amekubali suala la Chuo cha Serikali za Mitaa cha Hombolo mkoani Dodoma kwenda kufungua tawi Zanzibar kwa kuwa kitasaidia kujenga viongozi na wataalam katika masuala ya serikali za mitaa.

Licha ya pongezi hizo, Dk. Mwinyi alielekeza na kusisitiza kuendeleza kasi katika kushughulikia hoja zilizobaki za Muungano na ushirikiano katika kushughulikia masuala ya mazingira.

Waziri Jafo alimshukuru Rais Mwinyi kwa kikao hicho kizuri na msaada mkubwa anaowapatia katika kutimiza majukumu aliyopewa na Rais wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, katika kushughulikia masuala ya Muungano.

Pia alimshukuru Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa ushirikiano mkubwa anaompa katika kushughulikia hoja mbalimbali za Muungano.

Aidha, Jafo aliwashukuru Rais Samia na Dk. Mwinyi kwa imani yao juu yake na kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuimarisha Muungano na kuwaletea maendeleo wananchi wa Tanzania, wakiwamo wananchi wa Ugunja na Pemba.

Wengine waliohudhuria kikao hicho ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Marry Maganga, Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mohamed Hamis Abdullah, Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais na maofisa mbalimbali wanaoshughulikia masuala ya Muungano.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mawaziri wafanye uamuzi mgumu migogoro ya ardhi

**TIMU** ya Mawaziri wanane imekwenda katika vijiji mbalimbali nchini kufanya tathmini kuhusu migogoro ya ardhi inayohusu wananchi na hifadhi.

Hatua hiyo ni mwendelezo wa kazi hiyo ambayo walishaianza wakati wa uongozi wa awamu ya tano, ya kushughulikia migogoro sugu ya ardhi ambayo imekuwa ikisababisha uhasama kati ya wananchi na hifadhi.

Uamuzi wa timu hiyo kwenda katika vijiji zaidi ya 900 kwenye mikoa 10 kufanya tathmini ya kazi hiyo sambamba na kutoa maamuzi ni kufuatia agizo lililotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan lengo likiwa kuitafutia migogoro hiyo ufumbuzi wa kudumu.

Ndani ya wiki hii baada ya mawaziri kuanza kazi hiyo, Serikali imefuta mapori 12 yenye ukubwa wa ekari 707, 659 na misitu 12 ya ukubwa wa ekari 46,755, kwa ajili ya kuwapatia wananchi, kuendesha shughuli za uzalishaji mali zikiwamo kilimo na ufugaji.

Hayo yalibinishwa jana na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, wakati wa ziara ya mawaziri wanane wa kisekta kutoa mrejesho wa utatuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi katika vijiji 920.

Lukuvi alisema, tayari GN za Misitu na Mapori hayo, zimefutwa katika maeneo husika na sasa taasisi zenye dhamana na maeneo ya hifadhi zinatakiwa kulinda na kuweka alama za mipaka kwenye maeneo yaliyobaki kwa lengo la kuepusha kuvamiwa na wananchi.

Uamuzi huo umepokelewa kwa furaha na baadhi ya viongozi wa kisiasa na wananchi katika Wilaya Kondoa, mkoani Dodoma na kueleza kuwa ni uamuzi uliolenga kuwaonea huruma wakulima na wafugaji.

Kwamba ongezeko la watu linafanya kuwe na uhitaji mkubwa wa ardhi na uamuzi wa kuwabakisha wananchi unatoa huruma kwa kuwa kulikuwa na vijana wa maliasili waliotoa adhabu kali kwa wananchi walioingia maeneo ya hifadhi.

Kwa mujibu wa Lukuvi, katika vijiji 920 ambavyo timu ya mawaziri itapeleka mrejesho kuhusiana na utatuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi, kwa Mkoa wa Dodoma pekee vijiji vyake 40 kati ya 42, vilivyoingia maeneo ya hifadhi havitaondolewa na wananchi wataendelea na shughuli zao za kilimo na ufugaji.

Tunaridhishwa jinsi timu hiyo ilivyoanza tathmini hiyo kwa kasi na kufanya maamuzi ambayo yatawekwa kisheria, hivyo kuipatia ufumbuzi migogoro mingi ya ardhi katika vijiji vingi nchini.

Njia shirikishi ya kutumia mawaziri wengi bila shaka maamuzi yake hayataacha shaka yoyote tofauti na kama maamuzi hayo yangefanywa na waziri mmoja, na itakuwa vizuri kama migogoro ya ardhi itaendelea kushughulikiwa hivyo kutokana na ardhi kuwa ni suala mtambuka.

Tunaelewa kwamba utatuzi wa migogoro ya ardhi una vikwazo vingi kutokana na kugusa maslahi ya kila mmoja, lakini tuna matumaini kuwa mawaziri hao kila eneo watatoa maamuzi yasiyopendelea wala kuonea mtu yeyote zaidi ya kutanguliza maslahi ya Taifa.

Tunashauri kwamba serikali iufanye utaratibu wa kutumia timu ya mawaziri wa wizara hizo kuwa endelevu katika suala zima la utatuzi wa migogoro ya ardhi.

Moja ya sababu zinazochangia migogoro sugu ya ardhi ni wawekezaji wengi pamoja na matajiri kununua ardhi na kuihodhi bila kuiendeleza wakati wananchi wengi wana mahitaji kwa ajili ya kulima, kufuga pamoja na matumizi mengine.

Njia tunayoona kuwa inaweza kupunguza ukubwa wa tatizo hilo ni serikali kuweka muda maalum wa kuendeleza ardhi badala ya wamiliki kuihodhi na kugeuka kuwa mapori.00000000000

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com

ze'tichaz'dei




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Ukiendekeza haya, athari hizi kiafya zitakunyemelea

**MOJA** ya mtindo wa maisha uliozoeleka kwa baadhi ya Watanzania, ni kutokuwa na mwamko wa kupima afya zao kila mara, hadi pale wanapozidiwa na ugonjwa ndipo wanaanza kuhangaika kusaka matibabu.

Watu hao ndiyo wale ambao wakiugua maradhi mbalimbali, hawapendi kwenda hospitali kufanya vipimo au kupata ushauri wa wataalamu wa afya, badala yake wananunua dawa na kumeza.

Katika mazingira hayo, inaelezwa na wataalamu wa afya kuwa kumeza dawa bila kufanya vipimo au kupata ushauri wa wataalamu wa afya, kuna athari nyingi za kiafya kwa wahusika.

Pia kunatajwa madhara ya kutumia dawa bila ya kufanyiwa vipimo au ushauri wa daktari, ni matumizi holela ya dawa yanaweza kusababisha kifo, pia kuharibu baadhi ya seli za mwili na kuzifanya zigeuke kuwa seli za saratani, usugu wa maradhi na tatizo la mzio.

Mtaalamu Bingwa wa Magonjwa ya Binadamu wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (Mloganzila), Dk. Nzobendo Lucas, anashauri kuwapo mwamko wa kupima afya na kumeza dawa kwa kuzingatia ushauri wa wataalamu wa afya.

Sababu hapo ni kwamba, kuna athari mbaya tano zitokanazo na kumeza dawa au kunywa dawa, bila ya kufanyiwa vipimo vya kitaalamu, ili kujua tatizo kwanza kwa lengo la kuandikiwa dawa na tabibu kwa usahihi.

Miongoni mwa athari hizo zitokanazo na kutozingatia maelekezo ya wataalamu wa afya ni kifo, usugu wa maradhi, saratani, sumu mwilini na mzio, hivyo kwa nguvu zote kunashauriwa ziepukwe haraka iwezekanavyo.

Anabainisha kwamba, dawa ni sumu zinazokabili vimelea vya magonjwa na kwamba zinapimwa vibaya, hasa kwa kutopata ushauri wa kitabibu, kunaweza kusababisha athari hizo tano dhidi ya mtumiaji.

Katika ufafanuzi wake ni kwamba, kuna wakati mtindo huo huchangia vimelea vya ugonjwa kuzoea dawa husika na kusababisha ugonjwa usitibike na kubaki chanzo cha maradhi, kama vile malaria sugu au maambukizi katika njia ya mkojo, au iliyozoeleka UTI sugu.

Kimsingi, ushauri wa wataalamu wa afya ni muhimu kuzingatiwa, ingawa katika maisha ya 'uswahilini', watu hawana kawaida ya kupima afya mara kila mara na huenda kuna sababu za msingi zinazochangia hali hiyo.

Lililo bayana hapo, ni kutokana na hali duni ya uchumi, uelewa hafifu na sababu nyinginezo ambazo wanazijua wenyewe. Lakini, pamoja na hayo, suala la kuchunguza afya kwa mtu ni la msingi zaidi, kwa ajili ya usalama, kuliko kufanya mambo katika mtindo wa mazoea.

Hilo, pia ni vyema likaenda sambamba na kuachwa mtindo wa kujisikia maumivu au kuumwa na kwenda dukani kununua dawa na meza, hali inayoelezwa kuwa na athari kiafya.

Katika mwendelezo huo, mtu anakumbushwa kwamba, watu wenye maradhi kama ya moyo na shinikizo la damu, wanapaswa kuwa makini na dawa wanazozitumia, kwa kuwa zinaweza kuchochea matatizo yao na hatimaye vifo.

Ni kupitia ushauri huo, ni vyema sasa kila Mtanzania akawa makini kuzingatia mambo mawili ambayo kimsingi, yaani kuwa na mwamko wa kupima afya kila mara na umakini wa kutomeza dawa bila ya ushauri sahihi wa kitabibu.

Ni kwamba ingefaa kila mmoja wetu akaachana na kuishi au kufanya mambo kwa mazoea, hali inayohatarisha afya zetu kwa uzembe au kutokana na ukosefu wa elimu ya afya.

Wataalamu wa afya wamekuwa wakielekeza vitu vingi vya kuzingatia ikiwamo kutokatisha dozi, lakini ninaamini kwamba baadhi ya watu wamekuwa wakinywa dawa na kuishia njiani bila ya kuzimaliza walichoelekezwa na tabibu.

Mtindo huo wa kukatisha dozi umekuwa ukifanywa na baadhi ya watu wanaougua na tabibu kuwaandikia dawa, lakini wanapomeza na kuanza kupata unafuu, wanaziweka kando na kuendelea na maisha.

Nadhani umefika wakati kwa kila mmoja wetu kuwa makini na afya yake, ili kuepuka athari mbaya tano zinazoelezwa na wataalamu wa afya. Kikuu, tuachane na mazoea.

# TANGAZO

## THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
## PRESIDENT'S OFFICE-REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
## MPANDA MUNICIPAL COUNCIL

# FINANCIAL STATEMENTS FOR THE YEAR 2019/2020

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**PRESIDENT'S OFFICE - REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**
**MPANDA MUNICIPAL COUNCIL**
**STATEMENT OF FINANCIAL POSITION**
**AS AT 30th JUNE 2019**

| | Notes | 2019 TZS | 2018-Resteted TZS |
|---|---|---|---|
| **ASSETS** | | | |
| **Current assets** | | | |
| Cash and cash equivalents | 24 | 4,452,855,995 | 6,937,144,374 |
| Receivables and prepayments | 25 | 505,126,255 | 300,593,048 |
| Inventories | 26 | 261,293,582 | 268,783,490 |
| Other financial assets | 27 | - | - |
| | | 5,219,275,832 | 7,506,520,912 |
| **Non-current assets** | | | |
| Other financial assets | 27 | 34,389,944 | 27,593,296 |
| Investments in associates | 28 | - | - |
| Property, plant and equipment | 29 | 34,000,955,722 | 28,242,499,541 |
| Forest Asset | 33 | - | - |
| | | 34,035,345,666 | 28,270,092,837 |
| Non-current assets held for sale | 34 | - | - |
| **TOTAL ASSETS** | | **39,254,621,498** | **35,776,613,749** |
| **LIABILITIES** | | | |
| **Current liabilities** | | | |
| Payables | 35 | 972,209,130 | 679,766,441 |
| Employee benefits | 38 | - | 107,463,356 |
| Deferred income (Grant) | 11 | 381,287,985 | 32,208,929 |
| | | 1,353,497,115 | 819,438,726 |
| **Non-current liabilities** | | | |
| Long-term borrowings | 37 | - | - |
| Employee benefits | 38 | - | - |
| Provisions | 39 | 59,000,000 | - |
| Deferred Capital (Grant) | 41 | 3,994,351,518 | 5,333,555,883 |
| | | 4,053,351,518 | 5,333,555,883 |
| **TOTAL LIABILITIES** | | 5,406,848,632 | 6,152,994,610 |
| **NET ASSETS** | | **33,847,772,865** | **29,623,619,139** |
| **NET ASSETS** | | | |
| Capital/Taxpayers Fund | | - | - |
| Accumulated surplus/(deficit) | | 33,847,772,865 | 29,623,619,139 |
| Revaluation surplus | | - | |
| Minimum Compulsory Reserve | | - | - |
| **TOTAL NET ASSETS** | | **33,847,772,865** | **29,623,619,139** |

The financial statements were authorised for issue by the Board/Council/Management on 18.09.2019 and were signed on its behalf by:

Name: William P. Mbogo Title: Mayor Signature: ______

Name: MICHAEL F. [illegible] Title: MD Signature: ______

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**PRESIDENT'S OFFICE - REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**
**MPANDA MUNICIPAL COUNCIL**
***STATEMENT OF FINANCIAL PERFORMANCE - NATURE***
**FOR THE YEAR ENDED 30th JUNE 2019**

| | Notes | 2019 TZS | 2018-Resteted TZS |
|---|---|---|---|
| **Revenue** | | | |
| Taxes and levies | 9 | 1,125,022,771 | 1,103,007,801 |
| Fees, fines, penalties and licenses | 10 | 729,015,210 | 551,707,829 |
| Amortisation of revenue grants | 11 | 14,015,252,798 | 15,292,886,216 |
| Revenue from exchange transactions | 12 | 250,854,600 | 379,751,943 |
| Revenue from non exchange transactions | 41 | 6,274,084,829 | 6,516,921,630 |
| Finance income | 13 | 2,046,575 | - |
| Amortisation of capital grant | 41 | - | - |
| Other revenue | 14 | 615,164,360 | 195,145,434 |
| | | 23,011,441,142 | 24,039,420,853 |
| **Expenses** | | | |
| Wages, salaries and employee benefits | 18 | 13,046,362,280 | 11,949,147,481 |
| Supplies and consumables used | 19 | 2,351,593,239 | 1,120,695,697 |
| Maintenance expenses | 20 | 1,358,814,367 | 2,005,304,813 |
| Grants and other transfer payments | 21 | 1,376,529,163 | 1,272,988,577 |
| Finance costs | 22 | - | 67,815,754 |
| Impairment of receivables | | - | - |
| Provision for legal Case | 39 | 59,000,000 | - |
| Impairment of other financial assets | | - | - |
| Depreciation of property, plant and equipment | 29 | 594,988,367 | 1,490,971,228 |
| Impairment of property plant and equipment | 29 | - | - |
| Depreciation of investment property - carried at cost | 30 | - | - |
| Amortisation of intangible assets | 31 | - | - |
| Impairment of intangible assets | 31 | - | - |
| | | 18,787,287,416 | 17,906,923,550 |
| Share of associates surplus/(deficit) | | - | - |
| **Surplus/(deficit) during the year** | | 4,224,153,726 | 6,132,497,303 |
| **Attributable to:** | | | |
| Owners | | - | - |
| Non-controlling interests | | - | - |
| | | - | - |

Name: MICHAEL F. [illegible] Title: MD Signature: ______

Name: William P. Mbogo Title: Mayor Signature: ______

MUNICIPAL DIRECTOR MPANDA MUNICIPAL COUNCIL P.O. BOX 216-MPANDA

Lord MAYOR MPANDA MUNICIPAL COUNCIL P.O. Box 216 MPANDA-KATAVI

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**PRESIDENT'S OFFICE - REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**
**MPANDA MUNICIPAL COUNCIL**
**CASH FLOW STATEMENT - DIRECT METHOD**
**FOR THE YEAR ENDED 30th JUNE 2019**

| | Note | 2019 TZS | 2018 TZS |
|---|---|---|---|
| **Cash flows from operating activities** | | | |
| **Receipts** | | | |
| Taxes and levies | 70A | 1,125,022,771 | 1,103,007,801 |
| Fees, fines, penalties and licenses | 70B | 729,015,210 | 551,707,829 |
| Recurrent Grants | 11 | 14,238,944,103 | 14,984,430,146 |
| Revenue from exchange transactions | 70C | 351,968,448 | 379,751,943 |
| Finance income | 70D | 2,046,575 | - |
| Other income | 70E | 631,637,528 | 195,145,434 |
| Change in Miscellaneous Deposit | 24 | 9,242,499 | (49,238,523) |
| **Total Receipt** | | **17,087,877,133** | **17,164,804,630** |
| **Payments** | | | |
| Employee costs | 70F | 12,908,538,663 | 11,021,358,188 |
| Payments to suppliers | 70G | 2,523,308,043 | 1,389,479,187 |
| Maintenance expenses | 70H | 1,343,178,703 | 2,005,304,813 |
| Grants and other transfer payments | 21 | 1,376,529,163 | 1,272,988,577 |
| Finance costs | 22 | - | 67,815,754 |
| Other expenses | | 2,046,575 | |
| **Total payments** | | **18,153,601,147** | **15,756,946,520** |
| **Net cash from operating activities** | | **(1,065,724,013)** | **1,407,858,110** |
| **Cash flows from investing activities** | | | |
| Acquisition of property, plant, and equipment & investment properties | 29 | (6,353,444,829) | (3,764,612,853) |
| Acquisition of intangibles | | - | - |
| Investment with fixed deposit Receipts | | | |
| Receipts from sales of other long-term assets | | - | - |
| Payments to acquire equity/debt instruments of other entities | | | - |
| Receipts from sales of equity/debt instruments of other entities | | - | - |
| **Net cash from investing activities** | | **(6,353,444,829)** | **(3,764,612,853)** |
| **Cash flows from financing activities** | | | |
| Capital injected | | | - |
| Cash proceeds from issuing Government Stocks | | - | - |
| Cash proceeds from loans | | - | - |
| Cash proceeds from other short or long-term borrowings; | | | - |
| Cash proceeds from issuing other financial assets | | - | - |
| Cash payments for other financial liabilities | | - | - |
| Development grants received | | 4,934,880,464 | 7,689,096,408 |
| **Net cash used in financing activities** | | **4,934,880,464** | **7,689,096,408** |
| **Net increase in cash and cash equivalents** | | **(2,484,288,379)** | **2,364,758,362** |
| **Net foreign exchange difference** | | - | - |
| **Cash and cash equivalents at beginning of period** | 24 | **6,937,144,374** | **4,572,386,012** |
| **Cash and cash equivalents at end of period** | 24 | **4,452,855,995** | **6,937,144,374** |

**2.1 Report on the Audit of Financial Statements for the financial year ended 30th June, 2019**

**Unqualified Opinion**

I have audited the accompanying Financial Statements of Mpanda Municipal Council, which comprise the Statement of Financial Position as at 30th June, 2019 and the Statement of Financial Performance, the Statement of Changes in Net Assets Cash Flow Statement and the Statement of Comparison of Budget and Actual Amounts for the year then ended, as well as the Notes to the Financial Statements, including a Summary of Significant Accounting Policies set out in part 3.0 of this Audit Report.

In my opinion, the accompanying Financial Statements present fairly in all material respects, the Financial position of Mpanda Municipal Council as at 30th June, 2019, and its financial performance and its cash flows for the year then ended in accordance with International Public Sector Accounting Standards (IPSASs) accrual basis of accounting and in the manner required by the Public Finance Act, 2001 (revised 2004) and Local Government Finances Act 1982 (revised 2000).

**Basis for Opinion**

I conducted my audit in accordance with International Standards of Supreme Audit Institutions (ISSAIs). My responsibilities under those standards are further described in the Auditor's Responsibilities for the Audit of the financial statements section of my report. I am independent of Mpanda Municipal Council in accordance with the International Ethics Standards Board for Accountants' Code of Ethics for Professional Accountants (IESBA Code) together with the ethical requirements that are relevant to my audit of the financial statements in Tanzania, and I have fulfilled my other ethical responsibilities in accordance with these requirements and the IESBA code.

I believe that the audit evidence I have obtained is sufficient and appropriate to provide a basis for my opinion.

Charles E. Kichere
**CONTROLLER AND AUDITOR GENERAL**
**31st March, 2020**

National Audit Office,
Audit House,
4 Ukaguzi Road,
P.O. Box 950,
41104 TAMBUKARELI,
DODOMA. TANZANIA.
Tel: 255 (026) 2321759,
Fax: 255 (026) 2117527,
E-mail ocag@nao.go.tz
Website: www.nao.go.tz

# Hukumu ya Aveva, Kaburu Oktoba 21

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, imeahirisha hukumu ya aliyekuwa Rais wa Klabu ya Simba, Evans Aveva na Makamu wake, Godfrey Nyange, maarufu kama Kaburu.

Hukumu ya kesi hiyo iliyokuwa itolewe jana, mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Thomas Simba, sasa imeahirishwa hadi Oktoba 21, mwaka huu.

Kuahirishwa kwa hukumu hiyo, kumetokana na mshtakiwa Aveva kutokuwapo mahakamani, kwa sababu alikwenda kwenye matibabu.

Awali, upande wa Jamhuri ukiongozwa na mwendesha mashtaka wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Ipyana Mwakatobe, ulidai kuwa kesi hiyo imepangwa, kwa ajili ya kusomwa hukumu.

Hata hivyo, upande wa utetezi ulidai kuwa Aveva ameshindwa kufika mahakamani, kwa sababu amekwenda kwenye matibabu katika Hospitali ya Taifa Muhimbili.

Kutokana na madai hayo, Hakimu Simba alisema atasoma hukumu ya kesi hiyo Oktoba 21, mwaka huu na dhamana kwa washtakiwa inaendelea.

Mapema mahakamani hapo, upande wa Jamhuri ulifunga ushahidi wake ukiwa na mashahidi 10, dhidi ya washtakiwa.

Katika utetezi wake, Aveva alidai kuwa akiwa rais wa Simba mwaka 2014 mpaka 2017, ndani ya muda huo, klabu ilipata Dola 319,212, baada ya mauzo ya mchezaji Emmanuel Okwi kwenda klabu ya Etoile du Sahel ya Tunisia na aliitisha kikao cha kamati ya utendaji kuzungumzia matumizi ya fedha hizo.

Aveva alitoa madai hayo wakati akitoa ushahidi wake wa utetezi, dhidi ya kesi ya kula njama na matumizi mabaya ya madaraka katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba.

Aveva ambaye ni shahidi wa kwanza wa utetezi, alitoa ushahidi wake wakati akiongozwa na Wakili wa utetezi, Kung'he Wabeya.

"Katika kikao hicho, kamati iliamuru matumizi ya fedha hizo na kwamba zitumike katika ujenzi wa uwanja wa klabu Bunju na Dola 17,000 kati ya Dola 319,212 alipwe aliyekuwa mwenyekiti wa kamati ya usajili, Zachariah Hans Poppe, alizokuwa akiidai klabu yetu," alidai.

Katika kesi ya msingi, shtaka la kwanza, Aveva na Kaburu wanadaiwa kula njama na kutenda kosa la matumizi mabaya ya madaraka. Shtaka la pili, Aveva na Kaburu wanadaiwa kutumia vibaya madaraka yao kwa kuandaa fomu ya kuhamisha Dola za Kimarekani 300,000 kutoka kwenye akaunti ya Simba iliyoko Benki ya CRDB Azikiwe, kwenda kwenye akaunti binafsi ya Aveva iliyoko benki ya Barclays.

Katika shtaka la tatu, Aveva na Kaburu wanadaiwa kwa pamoja kughushi nyaraka iliyokuwa ikionyesha Simba inalipa mkopo wa USD 300,000 kwa Aveva kitu ambacho si kweli.

Pia Katika shtaka la nne, Aveva anadaiwa katika Benki ya CRDB kutoa nyaraka ya uongo ikionyesha Simba wanalipa mkopo wa USD 300,000. Pia anadaiwa kuwa katika Benki ya Baclays Mikocheni alijipatia USD 187,817 wakati akijua zimetokana na kughushi.

Katika shtaka la sita, Kaburu anadaiwa kumsaidia Aveva kujipatia USD 187,817 kutoka kwenye akaunti ya Simba wakiwa wanajua fedha hizo zimetokana na zao la kughushi.

Aveva na Kaburu wanadaiwa kughushi hati ya malipo ya kibiashara wakionyesha kwamba nyasi bandia zilizonunuliwa na Simba zina thamani ya USD 40,577 huku wakijua kwamba si kweli

Katika shtaka la nane, Aveva anadaiwa kuwasilisha hati ya malipo ya kibiashara ya uongo kwa Levison Kasulwa kwa madhumuni ya kuonyesha kwamba Simba wamenunua nyasi bandia zenye thamani ya USD 40,577

Shtaka la tisa, Aveva na Kaburu wanadaiwa kuwasilisha nyaraka za uongo kuonyesha kuwa Simba imenunua nyasi bandia zenye thamani ya USD 40,577.



Wafanyakazi wa Benki ya Exim, wakiongozwa na Mkuu wa Idara ya Huduma kwa Wateja wa benki hiyo, Frank Matoro (watatu kushoto), wakimkabidhi keki ya kumtakia heri ya mafanikio mmoja wa wateja wao, Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya Radi Service, Abdallah Hashim (wapili kushoto), walimpomtembelea mteja huyo, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya wiki ya huduma kwa wateja, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yafuta mapori 12, wananchi kuanza kunufaika

**Na Munir Shemweta,**
DODOMA

SERIKALI imefuta mapori 12 yenye ukubwa wa ekari 707, 659 na misitu 12 ya ukubwa wa ekari 46,755, kwa ajili ya kuwapatia wananchi, kuendesha shughuli za uzalishaji mali zikiwamo kilimo na ufugaji.

Hayo yalibinishwa jana na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, wakati wa ziara ya mawaziri wanane wa kisekta kutoa mrejesho wa utatuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi katika vijiji 920.

Lukuvi alisema, tayari GN za Misitu na Mapori hayo, zimefutwa katika maeneo husika na sasa taasisi zenye dhamana na maeneo ya hifadhi zinatakiwa kulinda na kuweka alama za mipaka kwenye maeneo yaliyobaki kwa lengo la kuepusha kuvamiwa na wananchi. Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Kondoa, Mohamed Kova, alipokea uamuzi huo wa serikali kwa furaha na kueleza kuwa ni uamuzi uliolenga kuwaonea huruma wakulima na wafugaji.

"Ongezeko la watu linafanya kuwe na uhitaji mkubwa wa ardhi na uamuzi wa kuwabakisha wananchi unatoa huruma kwa kuwa kulikuwa na vijana wa maliasili waliotoa adhabu kali kwa wananchi walioingia maeneo ya hifadhi," alisema Kova.

Kwa mujibu wa Lukuvi, katika vijiji 920 ambavyo timu ya mawaziri itapeleka mrejesho kuhusiana na utatuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi, kwa Mkoa wa Dodoma pekee vijiji vyake 40 kati ya 42, vilivyoingia maeneo ya hifadhi havitaondolewa na wananchi wataendelea na shughuli zao za kilimo na ufugaji.

Akiwa na timu ya mawaziri katika Kijiji cha Mwombotole, Lukuvi alisema vijiji viwili kati ya 42 katika Mkoa wa Dodoma, vitaondolewa kupisha ujenzi wa bwawa la maji la Farkwa. Alivitaja vijiji hivyo, kuwa ni Bubutole na Mwombose vilivyoko katika Wilaya ya Chemba.

Kwa mujibu wa Lukuvi, serikali tayari imeanza kulipa fidia na kubainisha kuwa wananchi ambao fidia haikwenda vizuri, serikali ipo na kila mtu lazima alipwe kulingana na mali zake na kusisitiza kuwa Rais Samia Suluhu Hassan alishatoa fedha, kwa ajili ya kujenga huduma za shule, zahanati na maji.

Tayari wakazi 2,829 sawa na asilimia 99 kati ya 2,868 katika vijiji hivyo viwili wameshalipwa fidia. Bwawa litakalojengwa litakuwa na ukubwa wa kilomita za mraba 68 na mililita za ujazo milioni 470 na litanufaisha wakazi wa jiji la Dodoma na wilaya za Chemba, Bahi na Chamwino pamoja na vijiji vyote vitakavyopitiwa na bomba hilo.

Aidha, Waziri Lukuvi alisema baadhi ya vitongoji kwenye vijiji 20 katika Mkoa wa Dodoma, navyo vitafanyiwa tathimini upya ili kuondoa kasoro zilizojitokeza awali na tathmini hiyo itakuwa shirikishi kwa viongozi, wataalamu na wananchi wa vitongoji husika.

"Vijiji vyote 40 katika mkoa huu wa Dodoma vitabaki ila ndani ya vijiji 20 kuna vitongoji tutavifanyia tathmini upya na suala hili litakuwa shirikishi. Maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan ni kuondoa shaka na taharuki kwa wananchi wanaoishi kwenye vijiji husika," alisema Lukuvi.

# Mbarawa ainyooshea kidole TRC mapato

**Na Mary Geofrey**

WAZIRI wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, ametaka Shirika la Reli Tanzania (TRC) kusimamia ukusanyaji wa mapato na kutoa mafunzo wa madereva wa treni ili kuepuka ajali za kudondoka kwa mabehewa zinazotokea mara kwa mara.

Prof. Mbarawa alitoa maagizo hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akipokea mabehewa 44 yenye thamani ya Sh. bilioni sita yaliyonunuliwa na TRC kupitia Mradi wa Kuboresha Usafirishaji wa Reli ya kati ya Dar es Salaam na Isaka (TIRP). "Kubwa ninalolitaka ni mapato. Tukikusanya fedha vizuri ndipo tutanunua mabehewa mengi zaidi, tutajenga reli za kisasa zaidi na kununua vichwa vingi vya treni. Huu ulikuwa msimamo wangu wa awamu ya tano na bado ni msimamo wangu wa sasa. Mimi sina mjomba, sina rafiki, rafiki yangu ni mapato, nendeni mkasimamie hili," alisema. "Kazi yetu kubwa ni kuhakikisha serikali inaingiza fedha nyingi kupitia miundombinu hii na tuendelee kuitunza ili tuitumie sisi wenyewe na vizazi vinavyokuja. Leo hii tunateremsha mabehewa 44 lakini litakuwa jambo la ajabu baada ya miezi sita yote yameanguka," alisisitiza.

Alisema kuna tatizo ama kwa wafanyakazi ambao wanatakiwa kupatiwa elimu au miundombinu ambayo inaendelea kufanyiwa maboresho na serikali. Aidha, aliahidi kuwa serikali itaendelea kutoa fedha kwa ajili ya kukarabati reli ya kati na kujenga reli mpya ya kisasa ili kuhakikisha sekta hiyo ndogo ya uchukuzi inapiga hatua.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa TRC, Masanja Kadogosa, aliahidi kusimamia na kutekeleza maagizo ya waziri ikiwamo ukusanyaji wa mapato. "Haya mabehewa mapya yatasaidia kuanzisha upya biashara ya makontena ambayo ilikuwa haipo, hivyo mapato yataongezeka na hatuendi kuua biashara ya malori isipokuwa tunawapunguzia safari ya kilometa 100. Kwa hiyo malori yaanzie safari Isaka yatembee Kilometa 30 tu badala ya kutembea Kilometa 130. Tumekuja kuleta neema kwa watu wa malori," alisisitiza Kadogosa.

Alisema behewa moja linabeba tani 46 za mzigo na mabehewa 20 yatasafirishwa kwa mara moja sawa na kusafirisha mzigo wa tani 920 kwa safari moja. "Hii ni sawa na malori 30 yenye uwezo wa kubeba tani 30 kila moja. Aidha, uwezo wa TRC kwa kutumia mabehewa haya mapya 44 utaongezeka sana na kupunguza kero ya msongamano wa mizigo bandarini na kupunguza uharibifu wa barabara kwa kiasi kikubwa," alisema Kadogosa.

Kuhusu mradi huo, alisema unatekelezwa kwa kutumia fedha ya mkopo wa Dola za Marekani milioni 300 kutoka Benki ya Dunia sawa na Sh. bilioni 600 ambao unahusisha maboresho miundombinu ya reli, ununuzi wa mabehewa na vichwa vya treni na mtambo wa ukaguzi wa njia za reli. Kadogosa alisema katika kutekeleza mradi huo, ukarabati wa kilometa 326 za njia ya reli toka Dar es Salaam hadi Isaka umekamilika pamoja na madaraja 374 na usanifu kwa ajili ya uboreshaji wa njia za reli kwenye bandari ya Dar es Salaam.

HABARI KITAIFA

# Naibu Waziri ataka kuimarishwa kamati za ulinzi wa mama, mtoto

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

NAIBU Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mwanaidi Ali Khamis, ameagiza kuimarishwa kwa kamati za ulinzi na usalama wa mtoto ili kukabiliana na vitendo vya ukatili.

Naibu Waziri alitoa agizo hilo jana jijini hapa wakati akizungumza na kamati za ulinzi wa mwanamke na mtoto pamoja kikundi cha malezi chanya zinazotekeleza Mpango wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili wa Wanawake na Watoto katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya

"Uzoefu unaonyesha maeneo vilipo vikundi hivi vya malezi vimekuwa na mchango mkubwa katika kuzuia ukatili na kutoa msaada kwa watoto walio katika mazingira hatarishi. Nitoe rai kwa watendaji wa ngazi zote washirikiane na kamati za MTAKUWWA kuhakikisha masuala haya yanayogusa wanawake na watoto yanashughulikiwa kikamilifu," alisema Mwanaidi.

Akitoa taarifa ya MTAKUWWA kwa niaba ya wenzake, Fransisco Mgwira, amesema wamefanikiwa kupunguza vitendo vya ukatili kwa kushirikiana na mamlaka zingine ikiwamo uongozi wa kata.

"Kamati imefanikiwa kutoa elimu ya ulinzi na usalama dhidi ya ukatili kwa watoto na wanawake katika shule za msingi na sekondari pamoja na kutambua mazingira hatarishi kwa watoto na kutoa maelekezo kwa viongozi namna ya kuwakinga watoto," alisema Mgwira.

Naibu Waziri pia alitoa wito kwa mamlaka zinazosimamia kesi za ukatili dhidi ya watoto na wanawake kusimamia uharakishaji wa kesi hizo na waathirika wapate haki zao.

Alisema kesi hizo za ukatili zikiachwa muda mrefu, zinapoteza ushahidi, hivyo wahusika wanakosa haki zao zinazostahili na kuzidi kuathirika kisaikolojia na kufanya jitihada za kutokomeza vitendo hivyo kusuasua.

Wakati huo huo, Naibu Waziri Mwanaidi aliwataka wazazi kushirikiana katika malezi na kuwajibika ili kuwalinda watoto ili kutofikia hatua ya kukinzana na sheria.

Awali, akiwasilisha taarifa ya shule hiyo ya maadilisho, msimamizi Justin Mjema alisema sababu kubwa za watoto kufikia hali ya kukinzana na sheria na hatimaye kupelekwa shuleni hapo ni migogoro ya familia, ndoa zilizovunjika au wazazi kutotimiza majukumu yao.

Naibu Waziri akiwa katika Hamashauri ya Wilaya ya Mbeya, alitembelea na kuona shughuli zinazofanywa na kikundi cha kinamama wajasiriamali cha Huyandola kinachojihusisha na kutengeneza chaki na kuagiza halmashauri kuendelea kukiwezesha kwa kukitafutia soko ili kurejesha mkopo kilioupata.



Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Festo Kiswaga (wa pili kushoto), akikabidhi cheti cha shukrani kwa niaba ya kampuni kwa Ofisa Uhusiano wa Jamii wa Barrick Bulyanhulu, William Chungu, baada ya kudhamini wajasiriamali zaidi ya 100 kushiriki katika maonyesho ya wajasiriamali ya Kangaroo, yaliyomalizika wilayani humo, juzi.. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kampuni yazindua huduma mpya bima

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Bima ya Phoenix imezindua huduma ya utulivu kwa lengo la kuwasaidia wateja wake wanapopata matatizo mbalimbali wakiwa kwenye vyombo vyao vya moto.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Phoenix, Ashraf Musbally, alisema juzi mkoani Dar es Salaam kuwa huduma hiyo ni ya bure kwa wateja wao wa bima kubwa ya magari (comprehensive).

Musbally alisema wamiliki wa vyombo vya moto wanakutana na matatizo mengi ikiwa ni pamoja na kuharibika kwa magari, kuishiwa mafuta, kusahau funguo na mengine ambayo kampuni hiyo itayatatua bila gharama yoyote.

"Lengo la kutoa huduma hii ni kuwapa utulivu wateja wetu wanapokabiliana na matatizo mbalimbali wakiwa barabarani na hata nyumbani kwao.

"Unaweza kukuta gari lako limekataa kuwaka, unachotakiwa kufanya ni kutoa taarifa kwetu na mafundi watakuja kukufanyia matengenezo hapo hapo nyumbani kwako," alisema Musbally.

Alisema mipango yao ni kutoa huduma hiyo mikoani ili wateja wao walioko katika maeneo hayo nao wanuafaike na na huduma hiyo siku za karibuni.

"Hii ni huduma ya ziada, haina malipo yoyote ambapo mteja wetu wa bima kubwa atafaidika nazo," alifafanua.

Meneja Mkuu wa Phoenix Assurance, Robert Kalegeya, alisema wameamua kutoa huduma hiyo kama faraja kwa wateja wao ili waendelee kufanya nao kazi.

Kalegeya alisema kuwa biashara ya bima ina ushindani mkubwa kutokana na uwapo wa kampuni nyingi nchini.

Alisema kuwa kutokana na ushindani huo, kampuni yao imeamua kuwa na ubunifu wa kutoa huduma mbalimbali ili kutoa huduma bora kwa wateja wao.

Meneja wa Leseni na Usimamizi wa Mwenendo wa Soko wa Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima Tanzania (TIRA), Hillard Maskini, aliipongeza kampuni hiyo ya bima kwa kuanzisha huduma hiyo.

Mkuu wa Kitengo cha Elimu kwa Umma cha Trafiki Makao Makuu, Mrakibu wa Jeshi la Polisi Mossi Ndozero, alisema huduma hiyo ina lengo la kudumisha usalama wa wateja ambao Jeshi la Polisi linasisitiza.

# Watafiti wapigiwa chapuo kwa kazi zao

**Na Dinna Maningo,** MWANZA

TUME ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) imesema kazi zinazofanywa na watafiti mbalimbali hapa nchini hazifahamiki kwa wananchi kutokana na lugha wanayotumia kuandaa taarifa hizo.

Hayo yalisemwa jana katika mafunzo ya waandishi wa habari na watafiti na Mkurugenzi wa Menejiment ya Maarifa katika Tume hiyo, Dk. Philbert Luhunga.

Kutokana na hali hiyo, Dk. Luhunga aliwataka waandishi wa habari kuziandika taarifa za sayansi, teknolojia na ubunifu na kuzitangaza lugha rahisi na inayotambulika na wananchi wengi ili kuchochea kasi ya utumiaji wa taarifa hizo.

Kwa kufanya hivyo, alisema hatua hiyo itasaidia kuchagia kwenye maendeleo endelevu ndani ya jamii.

Akitoa mada ya umuhimu wa utafiti na usambazaji wa matokeo ya utafiti kwenye mafunzo hayo kwa waandishi kutoka mikoa ya Mara, Kagera na Mwanza, Dk. Luhunga aliwata waandishi kuandika habari za utafiti ili kuisaidia jamii.

"Mfano watafiti wanafanya utafiti wa mbegu nzuri za kilimo lakini wananchi wanashindwa kuzitumia maana hawazifahamu.

Waandishi wa habari mkiandika habari za matokeo ya utafiti mtasaidia kazi za watafiti wa sayansi, teknolojia na ubunifu kutambulika
na kutumiwa na jamii" alisema.

Kaimu Katibu Tawala Mkoa wa Mwanza, Emilly Kasagala, alisema taarifa nyingi za utafiti zinafanyika zikiwamo za kilimo, lakini namna ya kuwafikia walengwa ambao ni wananchi bado ni tatizo.

Kasagala aliipongeza COSTECH kwa kutoa mafunzo hayo na kwamba yatawasaidia waandishi wa habari kuandika habari za kisayansi kwa lugha rahisi ambayo itawafikia wananchi kwa urahisi.

"Watafiti wamekuwa wakifanya utafiti mbalimbali wa kisayansi, lakini matokeo ya utafiti hayawafikii wananchi kwa wakati na hivyo baadhi ya tafiti kutokuwa na matunda mazuri ndani ya jamii, " alisema Kasagala.

Akieleza malengo la mafunzo hayo, Ofisa wa Programu ya Mafunzo kutoka COSTECH, Deusidedith Leonard, alisema wanaendesha mafunzo ya namna ya kuandaa na kuwasilisha taarifa za Sayansi,Teknolojia na Ubunifu (STU).

Alisema kuwa lengo lingine ni kuwapa uelewa wa kuwasilisha taarifa za kitafiti kwa lugha rahisi ili wanahabari waweze kuchakata na kufikisha taarifa hizo kwa walengwa wakiwemo watunga sera, wafanya uamuzi.

# Zaidi ya mbwa 400 wapata chanjo

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MBWA 438 na paka tisa katika Halmashauri ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga wamepatiwa chanjo ya kichaa cha mbwa ili kuwakinga na tatizo hilo ambalo limekuwa likileta madhara.

Akizungumza juzi mjini hapa, wakati wa kilele cha utoaji wa chanjo hiyo, Ofisa Mifugo wa Manispaa hiyo, Dk. Kija Daudi, alisema chanjo hiyo ilikuwa imetolewa bure kwa ufadhili wa Shirika la Kutetea Haki na Ustawi wa Wanyama (TAPO) katika viwanja vya Magereza.

Alisema jumla ya mbwa na paka 449 wamepewa chanjo hiyo na pia wamewapatia dawa za minyoo, vitamini na kutoa elimu ya uandaaji wa vyakula vyenye lishe kwa wanyama hao.

"Manispaa tunalipongeza Shirika la Tapo kwa kutoa chanjo hii bure kwa wananchi wetu wanaofuga mbwa na paka, hii itasaidia kwa kiwango kikubwa katika kupunguza tatizo la kichaa cha mbwa hasa kwa mbwa wanaozurura mitaani bila kuwa na wenyewe," alisema Dk. Daudi.

Ofisa mifugo wa shirika hilo, Dk. Davidi Sospiter kutoka kata ya Bulige, alisema kila mwaka hutoa huduma hiyo bila malipo ingawa mwitikio wa wananchi bado umeendelea kuwa chini tofauti na kipindi cha nyuma.

Alisema kuwa mwaka jana walitoa huduma hiyo kwa zaidi ya mbwa 800 na paka 50, lakini mwaka huu wamechanja mbwa 438 na paka tisa pekee jambo ambalo linaashiria wananchi hasa wafugaji hawana uelewa juu ya tatizo la kichaa cha mbwa na kuhitajika elimu.




Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Ng'wilabuzu Ludigija (kushoto), akipokea moja ya reflecta 2,000 kutoka kwa Mkurugenzi wa M-Pesa ya Vodacom, Epimack Mbeteni, jijini Dar es Salaam jana, zilizotolewa na kampuni hiyo kwa Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA), kwa ajili ya wakusanya malipo ya maegesho ya magari nchi nzima. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wapigwa marufuku kuandaa mashamba kwa kuchoma moto

**Na Francis Godwin,** IRINGA

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbalo, amepiga marufuku wananchi wanaozunguka misitu ya hifadhi ya taifa na hifadhi za taifa kuandaa mashamba kwa kuchoma moto bila kuwapo watu wa Wakala wa Misitu Tanzania (TFS).

Dk. Ndumbalo alitoa agizo hilo juzi baada ya kutembelea shamba la miti la Sao Hill, Wilaya ya Mufindi ambalo wiki iliyopita sehemu ya shamba hilo liliteketea kwa moto unadaiwa kumshinda mwananchi aliyekuwa akiandaa shamba lake kwa kuchoma moto nyasi.

Alisema kutokana na kadhia hiyo kuendelea kushika kasi hasa kipindi cha kiangazi, ameagiza wananchi wote wanaozunguka misitu na hifadhi za taifa kote nchini kutochukua uamuzi wa kufanya maandalizi ya mashamba yao kwa kuchoma moto kama hajatoa taarifa katika ofisi za serikali za vijiji ama ofisi ya TFS.

Akizungumzia vijiji 60 vinavyozunguka shamba la Sao Hill, alisema kuanzia sasa wananchi wa vijiji hivyo wanatakiwa kusitisha kuandaa mashamba yao kwa kuchoma moto hadi watakapo toa taarifa kwa Mkuu wa wilaya ama ofisi ya TFS kwa ajili ya msaada zaidi wa uandaaji wa mashamba yao.

Katika hatua nyingine Waziri Ndumbalo alitaka vyombo vya habari kuendelea kuelimisha wananchi kuwa sehemu ya uhifadhi sio ya kuingia holela na hapendi kuona wananchi wakiendelea kupigwa na askari wa hifadhi kwa kukiuka sheria ya uhifadhi.

Mkuu wa Wilaya ya Mufindi, Saad Mtambule, alisema agizo la waziri kuhusu udhibiti wa moto kwao ni utekelezaji na kuwa hatapenda kuona mwananchi yeyote ndani ya wilaya hiyo akichoma moto ovyo bila kuwa na kibali cha kuandaa shamba.

Alisema hivi sasa ofisi yake inaandaa mkakati wa kuzunguka katika maeneo yote ya vijiji 60 vinavyozunguka Msitu wa Taifa wa Sao Hill ili kutoa elimu pia kuendesha zoezi la kuwabaini wenye tabia ya kuchoma moto misitu ili sheria ichukue mkondo wake.

Meneja wa Sao Hill, Lucas Sabida, alisema shamba hilo limekuwa likichukua hatua mbalimbali za udhibiti wa moto na kuwa wataendelea kutekeleza maelekezo ya waziri juu ya tahadhari kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali za serikali kama JKT na wengine.

Aidha, alisema shamba hilo limeendelea kutekeleza malengo mbalimbali na sasa wanategemea kukusanya kiasi cha Sh. bilioni 52 kwa mwaka kutokana na mavuno ya miti.

## Ofisi serikali mtaa yafungwa kisa deni

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

VIONGOZI wa Serikali ya Mtaa wa Tangini katika Halmashauri ya Mji wa Kibaha, wamelazimika kutoa huduma kwa wananchi nje ya ofisi baada ya kushindwa kulipa kodi ya pango kwa zaidi ya miezi 10.

Huduma nje ya ofisi zilianza kutolewa Oktoba 4, mwaka huu, nne baada ya mmiliki wa jengo la ofisi kushindwa kuendelea kuvumilia kuwaruhusu viongozi kutumia jengo lake bila kulipa kodi.

Mwenyekiti wa Mtaa huo, Primin Gama, akizungumza na waandishi wa habari jana, alikiri ofisi hiyo kuwa inadaiwa zaidi ya Sh. milioni moja.

Gama alisema deni hilo limetokana na aliyekuwa mtendaji wa kata hiyo, Benedict Maganga, kutumia fedha za kodi kwa matumizi yake binafsi tofauti na yaliyokuwa yakiainishwa na viongozi wa mtaa huo.

Alisema wamekuwa wakitoa fedha benki kwa ajili ya malipo ya jengo la ofisi na mambo mengine ya maendeleo lakini aliyekuwa mtendaji alikuwa akizitumia kinyume cha malengo, hivyo kusababisha ongezeko la deni hilo na kufungiwa ofisi.

Mwenyekiti alisema baada ya kubaini kuwa fedha za mtaa zilikuwa zikitumika vibaya, walilazimika kumwita Maganga ambaye alikiri kuwa na matumizi tofauti na malengo ya fedha hizo wakati zinatolewa benki.

Alisema mtendaji huyo alikubali kulipa deni la Sh. 1,590,000 ndani ya miezi 11 na aliandika barua kwamba kuanzia mwishoni mwa uliopita angekuwa akiweka fedha kwenye akaunti ya mtaa huo.

Mjumbe wa Serikali ya mtaa wa Tangini, Jacob Kandelema, alisema hatua ya viongozi kuhudumia wananchi nje ya ofisi imesababishwa na aliyekuwa mtendaji wa mtaa huo kwa kutumia fedha za mtaa tofauti na makubaliano.

Msimamizi wa jengo hilo, Almas Batende, alisema amewafungia viongozi hao hadi pale watakapokamilisha kulipa deni la Sh. 1,330,000 ambalo ni malimbikizo ya kodi ya miezi 19.

Maganga alipotafutwa kuhusiana na tuhuma hizo alisema hawezi kuzungumzia suala hilo kutokana na kwamba tayari ameshahama katika kata hiyo.

ama
ALHAMISI OKTOBA 7, 2021
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 13

**Usafirishaji haramu wa binadamu unavyobeba hatari ya nafsi zao**



Ukurasa 12

**Makuu ya binti miaka 15 asiyejiweza tangu miezi 2, vyote kwa mama mjane**

## MIAMBA NA MAPOROMOKO YA KIMANI …

# Penye jiografia alikojificha Chifu Mkwawa pakiwapo miamba, mazingira ya kipekee



Askari mwongoza watalii, Leonard Mwakajange, akionyesha fuvu alilotumia Chifu Mkwawa, kwa ajili ya kufanyika maombi mbalimbali. **PICHA: CHRISTINA HAULE.**

**Na Christina Haule, Mbarali**

UNAPOTAJA maporomoko ya maji ya Kimani na Nyarugenge, ni kivutio na utalii wa kipekee ulio wazi kutembelewa na jamii yenye pango la Chifu Mkwawa Mkwavinyika, shujaa wa kabila la Wahehe.

Huyo anatajwa aliishi miaka 800, akijificha dhidi ya Wajerumani, kabla ya kujipiga risasi mwenyewe huko Kalenga, mkoani Iringa.

Askari Mwongoza watalii katika Pori la Akiba Mpanga Kipengere, iliyo chini ya Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA), Lenard Mwakajange, anatoa historia ya maporomoko hayo kwa waandishi wa habari, waliotembelea eneo hilo kushuhudia mambo ya kitalii mahali hapo.

Anasema umaarufu wa maporomoko hayo unatokana na kuwapo miamba mikubwa na miinuko iliyojipanga kama ngazi, kupendezesha maporomoko hayo.

Mwakajange anasema, Chifu Mkwawa aliishi katika pango la asili kuanzia mwaka 1891 hadi 1898, mahali kando na maporomoko ambayo ametumia maji yake kuoga, pia kufua vyuma kutokana na kuwapo kiwanda kidogo cha kutengeneza silaha za jadi na za kivita, ili kukabiliana na wapinzani wake.

Mwakajange anasema, kwenye maporomoko hayo ya Kimani na Nyarugenge, kumekuwa kivutio cha pango lililotumiwa na Chifu Mkwawa na ukambebesha umaarufu mkubwa, kutokana na kuwapo harufu ya mimea mbalimbali inayowavutia watalii wa ndani na nje ya nchi.

Anashauri, wananchi wazuru mahali hapo na kukagua mahali ambako pango la Chifu Mkwawa lilipo, tofauti na mengine kutokana na kuwa na umbo la bati, hata kuwezesha mvua za masika zinavyotiririka kwa wingi yanapita juu ya pango na kumwagika mbele ya pango, sehemu kubwa inagubikwa na maji.

Mwongoza watalii huyo anasema, hali ya maji kupita juu ya pango imechangia maisha ya Chifu Mkwawa kubaki salama na ndiyo imekuwa namna bora ya kificho hata hakukamatwa na Wajerumani waliomsaka.

Askari huyo anasema, katika eneo hilo la pango kuna fuvu la kichwa cha nyani, ambalo Chifu Mkwawa alilitumia kwa matambiko mbalimbali na kwa sasa jamii za makabila ya Wahehe, Wabena, Wakinga na Wahanji nao wamekuwa wakifika kuzuru na kufanya matambiko yao.

Mtaaluma huyo wa hifadhini, anapasifu kuwa mahali palipojaa utajiri wa maporomoko yenye maji mengi nyakati zote na miamba mikubwa, inayovutia.

Anapafafanua kwamba ni mahali ambako kumezungukwa na viumbe ndege na nyani wanaoogelea katika makundi ya koo tatu tofauti, huku kukiwapo mvuke mkubwa unaotokana na maji yanayopita kutoka kilele cha juu cha kwenye maporomoko hayo.

“Maporomoko ya maji ya Kimani yana takribani mita mia na hamsini na mabwawa mbalimbali yanayoleta ladha ya watu kuja kutembelea, kurekodi video mbalimbali, kuogelea, kujifunza miamba kwa wanafunzi,” anasimulia

Anaendelea kuhusu kinachovutia watu ni: “kuona wanyamapori kama nyani wa njano ‘yellow baboon’, ndege aina tofauti na ni eneo linaloruhusu makazi ya wanyama kama Tandala na Ngorombo.”

Mhifadhi Mwandamizi wa Pori la Akiba la Mpanga Kipengere, Alfred Kipondamali, anaeleza pori hilo lina zaidi ya maporomoko saba ya maji, yaliyoko katika maeneo tofauti maarufu na kwa sasa yalioendelezwa na kutumika kwa utalii ni Kimani na Nyarugenge.

“Hili pango ni sehemu maarufu sana kwa utalii na watu wamekuwa wakifika hapo. Tumelitunza, kwani ni pango zuri la kutalii na kuonyesha na historia katika nchi yetu,”aanasema.

Pango la Chifu Mkwawa, lilianza kutumika kama maficho wakati wa vita vya Wajerumani na Wahehe kati ya miaka ya 1855 hadi 1898 na kwamba pango pamoja na maporomoko hayo, yanapatikana katika eneo la Mbarali, jirani na barabara kuu ya Dar es Salaam - Mbeya

AFYA

# Makuu ya binti miaka 15 asiyejiweza tangu miezi 2, vyote kwa mama mjane

## •Mama atoka wodini, akuta msiba umeisha na mali zote

**Na Devota Mwachang'a**

NEEMA John, alizaliwa Novemba 15 mwaka 2006. akiwa mwenye afya na uzito mkubwa kilo 6.8. Ilikuwa siku ya furaha zaidi kwa wazazi wake, Lydia Selestine na John Amon, waliopata mtoto wao wa kwanza baada miaka saba ya ndoa.

Akiwa na umri wa miezi miwili tu, Neema aliugua na kupatwa na homa kali, akalazwa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) Chumba cha Uangalizi Maalum (ICU), kwa miezi miwili akiwa hajitambui.

Madaktari walithibitisha kuwa ubongo wake umeharibika kutokana na hali hiyo, hata akapatwa tatizo la mtindio wa ubongo. Ni aina ya tatizo linalosababishwa na jeraha la kudumu kwenye ubongo, kabla, wakati au baada ya kuzaliwa.

Ukimuona Neema amelala kitandani, ni vigumu kutambua umri wake ni miaka 15. Kisa? Ana aina ya ulemavu, hawezi kusongesha mwili wake kwa namna yoyote, amekuwa mtu wa kulala maisha yote, haongei, anafungua macho tu, ama kulia au kukoroma.

Yuko tofauti na watoto wengine, Neema hakuwahi kufurahia matendo na michezo ya kitoto ambayo mtoto yeyote wa rika yake anafanya.

Lydia, mama wa Neema, bado hajakubaliana na ulemavu wa binti yake umkatishe tamaa, hayuko tayari kumuacha bila uangalizi. Mwenyewe anafafanua:


“Mtoto huyu amebadilisha maisha yangu, yeye ni zawadi yangu kutoka kwa Mungu, nilitamani niisikie sauti yake akiniita mama, lakini haikutokea, angalau nikiitwa na watoto wengine nafarijika. Licha ya ugumu wote, tunashukuru maisha yanakwenda.”

Sikupata matatizo yoyote nilipokuwa mjamzito, ila nilikuwa na tumbo kubwa sana mithili ya mwenye mapacha. Ninachokumbuka nilikuwa na njaa, nilihitaji kula mara kwa mara.

Mtoto alikuwa mkubwa sana, nilijifungua kwa operesheni chini ya uangalizi wa Dk. Massawe (marehemu daktari bingwa wa watoto), ambaye ndiye alimwita jina la Neema binti yangu.

Mume wangu alikuwa dereva wa malori. Alihakikisha anafanya kila liwezekanalo, mwanawe apate matibabu. Alipambana sana, hata kumuomba daktari wampeleke mwanawe akatibiwe nje ya nchi, lakini waliwambia tatizo linalomsibu mtoto huyo lipo ndani ya uwezo wa madaktari wa MOI.

Baba yake Neema (marehemu John), alijitahidi sana kumhudumia mwanawe kwa miaka miwili tu halifariki dunia mwaka 2008 na kumuachia malezi ya mtoto peke yake hadi leo.



Lydia Selestine, akiwa amempakata mwanawe, Neema John. **PCHA: DEVOTA MWACHANG'A,**

### MAKUU AKITOKA WODINI

Anasema aliishi na mume wake kwa ndoa ya mwaka 1999 na kufanikiwa kujenga nyumba eneo la Tabata na kununua ardhi eneo la Mbezi jijini Dar es Salaam.

“Baada ya kumaliza mazishi ya Mume wangu, tukiwa bado msibani, hali ya binti yetu ilibadilika, akakamaa, alipatwa na homa kali hadi kuzimia, wasamaria wema wakatusaidia kutupeleka hospitali ya Muhimbili ambako tulilazwa kwa muda wa miezi Minne,” anasimulia.

Akiwa hospitalini, baba mkwe wake aliamua kujigawia mali zilizokuwa zinamilikiwa na marehemu pamoja na mkewe; aliuza nyumba na viwanja walivyomiliki.

Baada ya kuruhusiwa kutoka hospitalini, mama yake Neema alishangaa kuona wanaelekea barabara ya Nyerere badala ya kwenda Tabata, hakujua kuwa makazi yao yamebadilika na kuhamishiwa eneo kingine kama makazi mapya.

“Hali hiyo ilinishangaza, nilimuuliza mdogo wangu wa kike aliyekuwa anatuongoza aniambie nini kilitokea nilipokuwa hospitalini, akasema baba mkwe wangu aliuza nyumba na mali zetu.

“Lakini alimkabidhi baadhi vitu kikiwemo kitanda changu; ndipo alilazimika kutafuta chumba kimoja cha bei rahisi katika eneo la Banana.... lililopo wilayani Ilala tukahamia huko.

“Maisha hayakuwa sawa bila mume wangu, hali ilikuwa ngumu na bado ngumu sana. Mnamo 2015 nilihamia hapa mitaa wa Machimbo - Lumo eneo la Yombo Vituka wilayani Temeke, ambako ninaishi na mtoto wangu katika chumba hiki kimoja.

“Namshukuru mwenye nyumba amekuwa akinivumilia kwa hali yangu hata pale ninapochelewa kulipa kodi,” anasimulia.

### MALEZI NA MAISHA

Kimsingi, mtoto Neema anahitaji uangalizi wa muda mrefu. Ni hali inayomfanya mama yake ashindwe kujishughulisha na kazi zingine, vivyo hivyo hata fursa ya kuwa na mweza wa kiume.

Analifafanua hilo akisema: “Nimeamua kutokuwa na mwanaume kabisa baada ya kugundua...walijiengua kabla ya uhusiano kukomaa, baada ya kufahamu au kuona hali ya mwanangu mgonjwa.”

Mama huyo anasimulia kuwa maisha ya mtoto yamezidi kuyumba na kuna wakati, mama yake Neema amefikiria mabaya, akisimulia kupitia magumu yaliyomfikisha adiriki kuwa na fikra hasi mbele ya imani ya Mungu, hata sasa anajutia historia ya kuwa na utashi huo.

Kadri Mtoto Neema anavyokua, mama yake anasema ndivyo anavyozidi kukakamaa, anadhoofika na miguu yake inarefuka.

Anafafanua ugumu wake katika kumbeba mwanawe akiwa na simuzili kwamba miezi kadhaa iliyopita, akiwa anajiandaa kumpeleka hospitalini MOI, alihangaika kumbeba na akatereza sakafuni kisha kudondoka naye.

Mama huyo anasema, mtoto huyo alivunjika mguu wake mara mbili na akafungwa bandeji aina ya ‘POP’ na bado anaendelea kuhudhuria kliniki ya kumfanyia mazoezi ya viungo.

“Maisha yetu ni ya kutegemea misaada kutoka kwa wasamaria wema. Ikitokea mtu akatutembelea au kutukuta njiani, tukienda hospitali ananiwezesha kwa kiasi cha fedha, nanunua mahitaji.

“Wapo wengine wanatugawia chakula. Hivi karibuni kuna mtu alimnunulia neema dawa za tiba mbadala (supplements) za kuongeza madini mwilini, kuchua mwili na kusaidia misuli.

“Nawashukuru watu wanaonisaidia kwa njia mbalimbali, ili niweze kuendelea kumlea mtoto wangu. Kuna wakati waumini wa Kanisa Katoliki Jumuiya ya Mt. Bernadeta Parokia ya Yombo Vituka walinisaidia kwa michango ya fedha.

“Lakini, kwa namna ya pekee namshukuru sana Makamu Mwenyekiti wa Jumuia hiyo, Burchard Rwamtoga, yeye binafsi amenisaidia kwa mambo mengi hata kumkatia bima ya afya mtoto wangu ambayo inamsaidia hadi sasa,” anaeleza mzazi huyo.

### SHIDA ILIYOKO

Anitha Nathaniel, ni jirani anayeishi na mama yake, anakiri wako wenzake wanaompa ushirikianao mkubwa mama huyo na wapo ambao bado ni wazito katika utoaji ushirikiano huo.

Mama wa Neema anaendelea:”Mimi sina ndugu yeyote wa kunisaidia zaidi ya watu baki tu. Nina mdogo wangu (mwanamke) ambaye hali yake ni duni kama mimi. Baba yangu mzazi yupo hai, lakini ni mlemavu wa macho, hivyo hakuna namna tunayoweza kusaidiana.

“Nawaomba watu wenye mapenzi mema wataoguswa na hali tunayoipitia watusaidie. Neema anahitaji kwenda kliniki Muhimbili (MOI) kuangaliwa na kufanya mazoezi ya viungo mara tatu ndani ya juma, ila kutokana na kukosa pesa ya nauli wakati mwingine tunalazimisha kwenda angalau mara mbili tu.

“Tatizo lingine kubwa ni makazi. Hapa ninapoishi natakiwa kulipa kodi ya Sh. 35,000 kila mwezi na kwa sasa ninadaiwa zaidi ya Sh.100,000, ambayo ni kodi kuanzia mwezi Julai hadi sasa.

“Kama kuna mtu mwenye nyumba yake anaweza kunisaidia niishi na mtoto wangu, ama pia kunisaidia kulipa kodi nitashukuru sana. Naomba msaada wa hali na mali. “Neema hawezi kukaa, mgongo wake umepinda, amejikunja, hivyo ni vigumu kumkalisha. Anahitaji kufungwa mkanda asianguke, kwa kuwa ni wa kulala tu hawezi kukaa kwenye kiti cha magurudumu kama watumiacho

**Inaendelea Uk. 13**

AFYA

# Usafirishaji haramu wa binadamu unavyobeba hatari ya nafsi zao

**Na Zanura Mollel, LONGIDO**

- Jinsia kike wako hatarini maradufu
- Wadau Uhamiaji waainisha 'madudu'

USAFIRISHAJI haramu wa binadamu unabeba tafsiri ya kitendo au vitendo vya kukusanya, kusafirisha, kupokea na kuhifadhi mtu au watu bila ridhaa yake au yao kwa njia ya udanganyanyifu. Pia, kuna nguvu na vitisho kwa malengo ya kumtumikisha isivyo halali.

Pia, ndani yake kuna dhana 'magendo ya binadamu' kwamba ni usafirishaji wa mtu kutoka nchi moja kwenda nyingine, ili kujipatia fedha.

Hapo kuna tabia uhusiano wao unaisha pindi anayesafirishwa akivuka mpaka kuingia nchi nyingine, ilhali mara nyingi hakuna ridhaa ya anayesafirishwa kwa msafirishaji.

Katika matukio ya usafirishaji haramu wa binadamu, mtu anaweza akafanya ndani ya nchi husika, kutoka mkoa mmoja kwenda mwingine na biashara ya magendo ya binadamu, hufanyika kuvuka mipaka kati ya nchi moja kwenda nchi nyingine.



Kundi la wahamiaji haramu, katika mazingira tofauti chini ya ulinzi, baada ya kukamatwa. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

**BIASHARA INAVYOFANYIKA**

Wapo watu wengi wamejikuta wakisafirishwa kwa magendo na wanaishia katika mikono hatari ya kuuzwa kingono, wahanga wakubwa ni kinamama na watoto, vijana wenye nguvu na hata wenye ulemavu.

Matukio mengi ya usafirishaji haramu wa binadamu na magendo dhidi yao ni miongoni mwa matukio ya uhalifu kimataifa yanayopangwa kuvuka mipaka.

Ni tukio linalotajwa kuwa uhalifu wa pili kwa ukubwa duniani, baada ya dawa za kulevya, nyuma yake kukiwapo uuzwaji silaha na kila mahali yana mkono wa raia husika mahali inakofanyika, wanaoyasaidia makundi ya kihalifu kuvusha wahusika mipakani.

Takwimu za karibuni za Shirika la Umoja wa Mataifa linalohudumia Watoto na Wanawake (UNICEF), inataja kuwapo wastani wa watoto milioni moja kila mwaka ni wahanga wa tukio hilo.

Zipo takwimu zinazoeleza ufanyaji biashara hiyo haramu, inatoa kipato kwa waendeshaji kila mwaka wastani wa dola za Marekani bilioni 32, kwa mujibu wa Shirika la Umoja wa Mataifa Kuhusu Dawa za Kulevya na Uhalifu (UNODC).

Matukio ya uhalifu kuvuka mipaka inaelezwa kufanywa na watu wenye nguvu kiuchumi, wakiwatumia wenye hali ya chini kimaisha na kuna wakati kwa kushirikiana na wahujumu waliopo kwenye mfumo wa kiserikali.

Kimsingi, Idara ya Uhamiaji ndiye mhusika mkuu anayesimamia udhibiti wa matukio hayo kisheria kama usafirishaji watu kwa magendo, biashara ya dawa za kulevya, usafirishaji silaha, utumikishaji kingono na ugaidi.

**RAIA ANAHUSIKAJE?**

Ni zao la kukua soko la ngono duniani inayoendana na hitaji la wafanyakazi wa bei rahisi viwandani, shambani na majumbani, pia kuwapo ushindani kati ya masikini na matajiri wakisaka kukidhi matakwa yake.

Makundi hayo yanajihusisha na uhalifu huo kwa sababu yanatajwa kuwa chanzo kikubwa cha mapato duniani kwa haraka, mbali na dawa ya kulevya, huku kukionekana hasara zake bado ni kidogo.

Hata hivyo, inajulikana nyendo za athari ya biashara hizoni machafuko, uvunjifu wa amani na uingizaji nyenzo hatari kwa taifa na usambazaji magonjwa na dawa za kulevya kienyeji.

**HALI YA NCHINI**

Ofisa Uhusiano kutoka makao makuu ya Idara ya Uhamiaji nchini, Mrakibu Msaidizi Azizi Kirondomara, anasema usafirishaji haramu wa binadamu ndani na nje ya nchi upo nchini tena wakitumikishwa pasipo malipo stahiki, vivyo hivyo kuwapo wasichana wanaoangukia manyanyaso ya kijinsia.

Anasema katika baadhi ya maeneo duniani ambako kuna utumikishwaji viwandani, machimbo ya madini na mashamba, yapo matukio vijana wadogo wa kiume wanalazimishwa ngono na kinamama waliowazidi umri, maarufu 'sugar mummy.'

Takwimu anazorejea Ofisa Uhamiaji huyo, ni kwamba asilimia75 ya waathirika ni wasichana na robo waliobaki wavulana, huku asilimia 89 wana umri chini ya umri wa miaka 18. Kuhusu wanakotoka Mrakibu Kirondomara, anasema idadi kubwa ya waathirika huchukuliwa kutoka mikoa ya Iringa ambako wanapatikana asilimia 15; Kilimanjaro na Morogoro, kila moja asilimia tisa.

Anaitaja mikoa ya Dar es Saalam, Arusha na Zanzibar ina kiasi kidogo wanaoangukia katika utumishi wa majumbani wanaobeba zaidi ya nusu ya kundi hilo, kwa maana ya asilimia 55; machinga asilimia 12 na makahaba wa ngono asilimia saba.

Ofisa Uhamiaji huyo anaendelea:"Mtoto ni mtu yeyote mwenye umri chini ya miaka 18, upatikanaji, usafirishaji, uhamishaji, uhifadhi au upokeaji mtoto kwa lengo la unyonyaji itachukuliwa kuwa biashara haramu ya binadamu.

Kimsingi, ni vitendo ambavyo duniani kote hutambuliwa kisheria duniani kuwa ni kosa kwa kutumia Itifaki ya Umoja wa Mataifa (UN Protocol)."

**MDAU WA VITA**

Ofisa kutoka Shirika la Wahamaji Duniani (IOM), Halima Sonda, anaiambia Nipashe kuwa wanawake barani Afrika wanapitia mateso katika usafirishwaji, ikiwamo kubakwa, kupigwa na kutelekezwa katika maeneo hatari wanakokosa chakula na maji, hata wanapoteza maisha wanawake na watoto.

Anasema asilimia kubwa ya wanaosafirishwa hudanganywa kwenda kufanya kazi nzuri katika mataifa mengine na wanapofanikiwa katika mataifa hayo hawakuti ajira walizotarajia, bali kutumikishwa kingono.

Ofisa huyo anasema, mtu anapofikisha umri miaka 28 huondolewa katika madanguro na kutupwa mtaani, kwani wanatafsiriwa kuwa wamezeeka.

Hapo ndipo anasema wanaingia katika hatua nyingine ya kukamatwa kwa tuhuma za kuingia humo pasipo kuwa na vibali, hivyo wanaangukia tuhuma mpya.

Anasema, kuna hatua nyingine za zama hizo wanawake hutumika katika matukio ya kigaidi wakiwapa ushirikiano makundi ya kialifu, wanaume wakiwatumia kama wake zao.

**KILICHO MPAKANI**

Tanzania imezungukwa na takribani mataifa nane, ambako kuna matukio uvushaji haramu binadamu, pia hata baadhi ya vitu visivyo halali kisheria.

Mwenyekiti wa bodaboda katika mpaka wa Namanga, Omary Zuaku, anasema usafiri mkubwa unaotumika zaidi ni pikipiki na anakiri baadhi ya waendesha badaboda, ndio wamekuwa wasafirishaji wa wahamiaji haramu, ama kwa kujua au kutojua.

---

# Makuu ya binti miaka 15 asiyejiweza tangu miezi 2, vyote kwa mama mjane

Inatoka Uk. 12

walemavu wengine," anaeleza.

"Natamani ningepata simu kwa ajili ya mawasiliano. Kuna wakati daktari wangu Muhimbili (MOI) anahitaji kunipa maelekezo kuhusu Neema, au mimi nahitaji kumuuliza jambo ninapoona hali ya mtoto imebadilika ghafla, lakini sina simu ya kuniwezesha kufanya hivyo," anasema.

**TABIBU BINGWA**

Bingwa wa tiba za magonjwa ya mfumo wa fahamu kwa watoto kutoka MOI, Dk. Edward Kija, anasema maradhi nayo yanaathiri ubongo wa mtoto wakati haujakomaa vizuri. Huwa unapata madhara ya kudumu, iwapo unakosa damu au oksijeni ya kutosha.

"Tatizo la ubongo humpata mtoto ndani ya miaka miwili tangu kuzaliwa. Hakuna tiba ya upasuaji wala dawa ya kuondoa madhara kwenye ubongo ulioathirika," anaeleza.

Dk. Kija anasema wataalamu wa afya wanasisitiza zaidi kumkinga mtoto ili kuhakikisha kabla ubongo haujakomaa vizuri, hapati madhara alitaja mbinu kuwa: "Mama mjamzito aende kliniki mapema na kufuata ushauri wa kitabibu.

"Pia, uchungu unapoanza mjamzito awahi hospitalini, kwani uchungu pingamizi ni hatari humfanya mtoto kuchoka na kushindwa kupumua vizuri." Anasema viwango vya kuathirika ubongo vinatofautiana kwa aliyeathirika sana hushindwa kutembea, hivyo anahitaji kupatiwa kiti maalum cha magurudumu kusaidia mgongo na shingo kuepuka asipate kibiongo na madhara zaidi.

Tatizo lingine analitaja ni mhusika kupata ama kifafa au degedege, hivyo inamhitaji kupatiwa dawa za kutumia kila siku kukabiliana na tatizo hilo. Pia, anasema mtoto mwenye tatizo hilo anahitajiwa kuonana na mtaalamu maalum aitwaye 'speech therapist' anayemsaidia kumeza chakula na kupunguza kupaliwa, kwani anapopaliwa kila mara anaweza kupatwaa na maradhi ya niumonia, hata akaishia kulazwa kila mara.

Dk. Kija anasisitiza kwamba kumuuguza mwenye maradhi hayo ya 'CP' ni gharama kubwa, hivyo msaada wa kifedha unahitajika katika kumhudumia kwa dawa, pia mazoezi ya viungo yanayosaidia misuli kukaza.

**Watakaoguswa na kuhitaji kumtembelea, kuonana au kuwasaidia wahitaji hao, wawasiliane kwa simu namba: +255 756 507 533 au +255 673 266 170.**

AFYA

## MIAKA 20 BIMA YA AFYA - NHIF

# Yanajinasibu kilele cha mafanikio, huku ikikiri 'milima na mabonde' bado mingi

- Wanyonge wabuniwa 'Akaunti Dunduliza'
- Usanii wa madai na elimu duni bado shida!

**Na Maulid Mmbaga, aliyekuwa Dodoma**

MWAKA 2001, serikali ilianzisha Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), kuwawezesha Watanzania kupata huduma bora za matibabu.

Umuhimu wake umeendelea kujidhihirisha katika mwitikio wa wananchi kujiunga na huduma hizo, ili kupata uhakika wa huduma tiba.

Mkurugenzi wa Rasilimali Watu na Utawala wa NHIF, Charles Lengeju, anasema katika maadhimisho ya miaka 20 ya mfuko, kwamba walianzisha ofisi za mikoa mwaka 2013, lengo ni kusogeza huduma kwa wahitaji waliko, sasa zikiwapo 30, Tanzania Bara na Zanzibar.

Lengeju anafafanua, kuna mtandao wa ofisi za mikoa unaosaidia kutoa huduma haraka, sambamba na kushughulikia vikwazo vinavyojitokeza katika utoaji huduma.



Aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Geita, Injinia Robert Gabriel, alipokalia kitanda kwa lengo la kukagua ubora wake, kilicho tolewa na NHIF, kwa hospitali ya mkoa huo.

**MICHANGO 'DUNDULIZA'**

Anasema, NHIF imejiboresha kwa kuanzisha mpango maalum wa malipo ya michango kwa awamu, ujulikanao 'dunduliza' ili kuwawezesha wenye vipato visivyokidhi malipo ya awamu, ikifanyika kupitia akaunti maalum ya benki.

Anafafanua 'dunduliza' hutumika zaidi kwa wanachama wanaojiunga kupitia vifurushi anavyovitaja kwa majina ya: Najali Afya, Wekeza Afya na Timiza Afya na dira iliyoko ni kuboresha mfumo kuyafikia makundi mengine.

Kwa mujibu wa Ofisa Utumishi huyo wa NHIF, baada ya hatua hiyo, mchango unawasilishwa kwenye mfuko kupitia utaratibu wa malipo wa serikali (GePG).

**MABORESHO YALIVYO**

Mkurugenzi wa Huduma za Wanachama wa NHIF Dk. Christopher Mapunda, anasema katika kupanua wigo wa wanachama, wamejumuisha makundi mbalimbali kama wabunge, wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, wajasiriamali na, wafanyakazi wa kampuni binafsi.

Pia, anawataja watu binafsi, wanafunzi wa vyuo na shule, wanachama wa vyama vya ushirika, kwa kushirikiana na taasisi za fedha na makundi ya wajasiriamali.

"Idadi ya wanachama wachangiaji imeongezeka kutoka wanufaika 691,774 mwaka 2001/2002 hadi kufikia wanufaika milioni 4.3 mwezi Machi mwaka huu sawa na asilimia nane ya Watanzania wote," anasema Dk. Mapunda.

Anataja idadi ya wachangiaji kwenye mfuko, wanaojiunga kwa mujibu wa sheria ni asilimia 46 na wa hiari asilimia 54.

Mapunda anasema wanachama wake hupata vitambulisho vya matibabu kwa wakati, kwani imekasimu uandaaji kwa ofisi za mikoa, hatua inayotajwa kuongeza ufanisi, vikiwafikia wahitaji ndani ya siku tano, kinyume na zamani ilichukua mwezi mmoja.

Anabainisha hadi mwezi Machi mwaka huu, mfuko ulishasajili vituo vya matibabu 9,152 nchini kote, kuanzia ngazi ya zahanati hadi hospitali ya rufani za taifa, pia maduka ya dawa na kliniki maalum.

"Kati ya vituo hivyo, vya serikali ni 6,292 ambavyo ni sawa na asilimia 69, vya mashirika ya dini ni 909 sawa na asilimia 10, na vituo vya watu binafsi ni 1,951 sawa na asilimia 21.

"Katika kuhudumia makundi maalum yenye uhitaji wa huduma za uokozi, mfuko umeingia mkataba na kampuni zinazotoa huduma hizo," anasema Dk. Mapunda.

Anafafanua kuwa, mfuko unaendelea kuboresha mafao yake kwa mwanachama na hadi sasa ni maeneo ya kugharamia: Ada ya uandikishaji na kumuona daktari; vipimo vikubwa na vidogo; dawa za aina tofauti kulingana na miongozo ya tiba nchini; gharama za upasuaji mdogo na mkubwa; na ule wakitaalam unaofanywa na madaktari bingwa.

Gharama nyinginezo za tiba ni: Mgonjwa kulazwa; afya ya kinywa na meno; macho na miwani; vifaa saidizi; mazoezi ya viungo (physiotherapy); huduma maalum za magonjwa yasiyoambukiza kama vile moyo, figo na saratani.

Pia, kuna maboresho katika huduma za kibingwa zikiwamo matibabu ya moyo, kusafisha damu, saratani, upandikizaji viungo na kugharamia vipimo vikubwa (MRI na CT Scan).

Zingine anazitaja ni kupeleka madaktari bingwa katika maeneo ya pembezoni penye uhitaji, pia kuongeza idadi na aina za dawa na vipimo muhimu, ili kukidhi mahitaji ya tiba kwa wanachama.

"Huduma hizi zimeendelea kuboreshwa kwa kuzingatia tathmini ya uhai na uendelevu wa mfuko, mahitaji ya huduma za matibabu nchini, maoni kutoka kwa wadau pamoja na maendeleo ya teknolojia ya tiba," anafafanua Dk. Mapunda.

**ELIMU KWA UMMA**

Dk. Mapunda anafafanua namna NHIF inavyotekeleza mpango wa uhamasishaji elimu ya umuhimu wa upimaji afya kwa umma; kujiepusha na magonjwa; kuongeza usajili wa vituo vya kutoa matibabu vya serikalini na binafsi, vilivyopo mjini na vijijini.

Pia, anasema mfuko unaboresha huduma za mikopo inayotoa katika maeneo kama: vifaa tiba, kukarabati vituo vya afya, dawa na vitendea kazi, hali kadhalika ikiboresha mifumo ya teknolojia ya habari na mawasiliano katika vituo husika vya afya.

**PENYE UGUMU**

Daktari Mapunda anataja magonjwa yanayougharimu mfuko zaidi ni saratani na figo, akitaja wastani wa gharama zake, tiba ya saratani kila mwaka ni zaidi ya Sh.milioni 69.9; kusafisha damu, Sh. milioni 35.8; na upasuaji mkubwa wa moyo Sh.milioni 12.5.

Pia, anasema wapo wanaojiunga na NHIIF pale wanapoumwa; wapo watoa huduma za afya kutozingatia miongozi ya tiba; na kuongezeka magonjwa sugu yasiyoambukizwa.

Eneo lingine Dk. Mapunda analitaja ni kuongezeka kwa gharama za matibabu nchini, uwasilishaji madai yenye viashiria vya udanganyifu kutoka vituo vya huduma; na kukosekana elimu ya hiari kujiunga na bima afya, ambayo makundi ya kijamii yanakosa.




Wananchi wakipata huduma za usajili katika ofisi za NHIF, zilizopo jijini Dar es Salaam. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

**UMUHIMU WA BIMA**

Mganga Mfawidhi wa Kituo cha Matibabu cha Decca jijini Dodoma, Dk. Gaudence Mathew, anasema kuwapo bima ya afya nchini ndio kumewezesha hospitali nyingi kujiendesha, akitoa wastani wa asilimia 80 ya wagonjwa wanaowatibu wana kadi za bima.

"Mfuko wa Bima ya Afya, pia umewezesha uhakika wa matibabu na upatikanaji dawa katika vituo vya kutoa huduma. Miaka ya hivi karibuni vituo vingi vilikuwa vinashindwa kujiendesha kutokana na ukosefu wa fedha, lakini uwapo mkataba wa huduma baina ya NHIF na vituo utoaji huduma umeimarika.

"Maboresho pia yamefanywa na NHIF katika eneo la mikopo kwa watoa huduma za matibabu kwa kutoa mikopo ya vifaa tiba, uboreshaji wa majengo na dawa katika vituo, ili kuhakikisha wanachama wanapata huduma bora," anasema Dk. Mathew.

Shabani Msuya, mkazi wa Ilala jijini Dar es Salaam, anasema bima ya afya zinaurahisishia umma matibabu kirahisi, akitoa mfano awali alitumia zaidi ya Sh. 70,000 kila alipomfikisha mtoto hospitali, lakini baada ya kujiunga na bima ya afya, anashuhudia nafuu ya matibabu.

Mkazi wa Gongolamboto, Dar es Salaam, Esther Bakari, ambaye ni mwanachama wa NHIF, anasema alianza kuona umuhimu wa bima hiyo wakati alipoanza kumuuguza mama yake, mgonjwa wa kansa ya koo.

Anasimulia namna mama yake alipata huduma za tiba bila ya usumbufu, akifafanua: "Kwa hali ya maisha ilivyo, tusingeweza kumudu gharama za matibabu yake, kwani alipewa huduma zikiwamo za dawa na nyingine ambazo gharama zake ni za juu."



## Waislamu wachagizwa ujenzi nyumba za ibada

**Na Peter Mkwavila,** BAHI

WAUMINI wa dini ya Kiislamu wilayani Bahi wameshauriwa kujitolea kujenga nyumba za ibada badala ya kutegemea wahisani kutoka nje.

Sheikh wa Wilaya hiyo wa Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA), Suleiman Twalib, alisema hayo alipokuwa akizungumza na waumini wa kata ya Chibelela kwenye uzinduzi wa ujenzi wa msikiti wa Chibelela.

Twalib alisema waumini hao wanapaswa kujitolea zaidi katika shughuli hizo ya kidini na kutumia nguvu kazi yao wenyewe badala ya kusubiri misaada kutoka huko nje.

"Hivyo ninawaomba ninyi Waislamu wa hapa Chibelela kuonyesha mfano wa ujenzi wa msikiti huu kwa kutoa michango yenu ya kifedha, nguvu zenu, mifugo, chakula ili kukamilisha kwa wakati badala ya kusubiri wafadhili waje wawajengee hapa," alisema.

Aliwataka viongozi wa kisiasa kuacha tabia ya kujiingiza kwenye imani za kidini, badala yake wawe mstari wa mbele katika kuhakikisha amani, upendo na umoja.

Alisema bado kuna baadhi ya viongozi wa kisiasa wamekuwa wakijiingiza kwenye imani za kidini na kuchochea migogoro hali ambayo imekuwa ikiwakosesha amani kwa waumini.

"Hapa lazima niseme hawa viongozi wa kisiasa wanaovuruga na kuhatarisha uvunjivu wa amani ikiwamo na kusababisha migogoro, kwetu sisi waumini tunawaona ni maadui tu, hivyo ninawaomba wajiepushe na tabia hiyo," alisema.

Imam Alfani Bwanzi akisoma risala kwenye uzinduzi huo, alisema ujenzi wa msikiti huo utajengwa kwa nguvu kazi ya waumini kwa kutoa mali na fedha.

# Waziri ataka utafiti wa mila zinazochangia maambukizi VVU

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Bunge, Kazi, Ajira na Vijana, Jenista Mhagama, ametaka kufanyika kwa utafiti wa kubaini mila hatarishi kwa jamii ili kuondokana nazo kutokana na kuchangia kuenea kwa maambukizi ya Virusi vya Ukimwi(VVU) na kuathiri wanawake na wasichana.

Mhagama aliyasema hayo jana jijini hapa kwenye kikao cha Kamati ya Bunge inayoshughulikia masuala ya Ukimwi na dawa za kulevya ilipokutana na Tume ya Kudhibiti Ukimwi (TACAIDS) kwa ajili ya kujadili vikwazo vya ukatili wa kijinsia, usawa wa kijinsia na mila potofu katika mwitikio wa kupambana na VVU/Ukimwi nchini.

Alisema utafiti huo ukifanyika utasaidia kubaini mila nzuri ambazo zitaendelezwa na mila potofu ambazo elimu itatolewa kwa jamii ili kubadili fikra na kuziondoa.

"Utafiti ufanyike na uonyeshe mwenendo wa mila ukoje kwa sasa. Pia wanawake watumike kuhamasisha wenzi wao kufanya tohara. Hili linasisitizwa kwa sababu suala la saratani ya mlango wa kizazi na maambukizi ya VVU vyote vinatokana na kujamiiana," alisema.

Awali, akiwasilisha mada kuhusu hali ya maambukizi ya VVU kwa mtazamo wa kijinsia, sababu na baadhi ya mila hatarishi, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa TACAIDS, Dk. Jerome Kamwela, alisema kumekuwapo na tofauti katika kiwango cha maambukizi katika mtazamo wa kijinsia.Alifafanua kuwa hadi mwaka 2017 kiwango cha maambukizi kilikuwa kikubwa miongoni mwa wanawake wenye umri kati ya miaka 15 na 49 kwa asilimia 5.7 ikilinganishwa na wanaume wa kundi hilo hilo kwa asilimia 3.5.

"Baadhi ya sababu zinazoelezwa kuchangia kuwaweka wanawake na wasichana balehe katika hatari kubwa ya maambukizi ni pamoja na kushamiri kwa mila hatarishi na mifumo ya kijamii na kiuchumi inayowabagua wanawake na wasichana," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema mila hizo hatarishi ni baadhi ya jamii kuendelea kutekeleza vitendo vya ukatili wa kijinsia kama ukeketaji na ndoa zisizo za hiari na za utotoni.

"Pia kukosekana kwa usawa wa kijinsia katika mgawanyo wa fursa za kiuchumi kunakosababisha wanawake wengi kuwa maskini wa kipato," alisema.

Alisema asilimia 29.4 ya wanawake waliowahi kuolewa au kuwa na wenza wenye umri kati ya miaka 15-49 wamewahi kushuhudia matumizi ya nguvu au unyanyasaji wa kingono kutoka kwa wenza wao.

Alitaja mikakati sita ikiwamo kuendelea kuchambua na kubainisha mila na desturi hatarishi zinazobagua wanawake katika maeneo mbalimbali ili kutafutiwa suluhisho.

Mweyekiti wa Kamati hiyo, Fatuma Toufiq, alitaka kuwapo na mkakati kwa vyombo vya habari wa masuala ya jinsia na Ukimwi ili kuwafikia wananchi wengi hasa vijana.

Alisisitiza kuwapo na uhamasishaji wa kuwashirikisha wanaume kupima VVU huku akiwataka wajumbe wa kamati hiyo wanaume kuwa mstari wa mbele kampeni ya kuhamasisha kupima.




Mkurugenzi Mtendaji wa Songas, Anael Samuel (kulia), akikabidhi mfano wa hundi yenye thamani ya zaidi ya sh. milioni 29 kwa mmoja wa viongozi wa jamii kutoka Kisiwa cha Songo Songo, katika hafla iliyofanyika kwenye kiwanda cha umeme cha Ubungo, mkoani Dar es Salaam hivi karibuni. Msaada huo, unakusudia kuwezesha utekelezaji wa mipango anuwai ya maendeleo katika kisiwa hicho, pamoja na ukarabati wa usafiri wa boti kwa dharura, utoaji wa walimu wa muda, na ukuzaji wa uwanja wa michezo wa kujiongezea mapato. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# CWT yawataka walimu kuwa wavumilivu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

CHAMA cha Walimu Tanzania (CWT) kimewataka walimu kuwa na subira kuhusu ahadi ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kuwaongezea mishahara aliyoitoa mwaka huu kwenye maadhimisho ya Sikukuu ya Wafanyakazi iliyofanyika kitaifa mkoani Mwanza.

Aidha, kimesema takwimu za Mpango wa Maendeleo ya Duniani zinaonyesha kuna upungufu wa walimu milioni 69 duniani.

Kaimu Rais wa CWT, Dinnah Mathaman, aliyasema hayo juzi jijini hapa katika maadhimisho ya Siku ya Walimu Duniani yaliyoandaliwa na CWT Mkoa wa Dodoma.

Alisema walimu wana kila sababu ya kuchapa kazi kutokana na serikali kuwajali katika masuala yao ya kila siku ikiwamo upandishwaji wa madaraja na ulipaji wa madeni, hivyo wanapaswa ahadi ya uongezwaji mishahara iliyotolewa na Rais.

Alisema lengo lao ni kuona walimu wanafanyia kazi kwa bidii ili kuisaidia serikali kuinua kiwango cha elimu nchini.

Hata hivyo, aliwataka walimu kukabiliana na kero mbalimbali wanazokutana nazo ili kuhakikisha zinakwisha na kufanya kazi kwa mujibu wa kanuni, taratibu na sheria zilizopo.

Akizungumza kuhusu upungufu wa walimu, alisema hilo ni tatizo la kidunia na kuwataka kufanya kazi kwa bidii.

Naye Jaji Mathew Mwalimu kutoka Sekretarieti ya Maadili, alisema walimu ni kada muhimu na hakuna kiongozi yeyote ambaye hajapita kwenye mikono ya mwalimu hivyo walimu wana kila sababu ya kukuona wao ni mstari wa mbele katika kuinua taifa.

Alisema hata yeye taaluma yake ni mwalimu kabla ya kuwa jaji, hivyo uwapo wake katika maadhimisho hayo ni kama sekretarieti ya maadili inayojihusisha na kutoa matamko mbalimbali.

Aliwapongeza walimu kwa kuadhimisha siku yao huku akiwataka kuendelea kufanya kazi kwa bidii ili kuhakikisha sekta ya ualimu inasonga mbele.

"Walimu msijione wanyonge na badala yake mnapaswa kutembea kifua mbele maana watu wote wakiwamo viongozi wakubwa wamepita kwenye mikono yenu na kuwapo hapo waliopo," alisema.





# DC ataka umeme kituo cha afya

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI wilayani Mbeya imeliagiza Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kuunganisha umeme katika Kituo cha Afya cha Ikukwa ambacho kimejengwa na serikali kwa zaidi ya Sh. bilioni 1.2 ili vifaa vya matibabu vilivyopo vifungwe na wananchi waanze kupata matibabu.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashid Chuachua, alito agizo hilo juzi alipoambatana na Mbunge wa Mbeya Vijijini, Oran Njeza, kufanya ukaguzi wa kituo hicho kilichoko katika Kata ya Ikukwa. Alisema kazi hiyo inapaswa kukamilika kabla ya Desemba mwaka huu.

Dk. Chuachua alitoa agizo hilo baada ya kuelezwa na Njeza pamoja na baadhi ya viongozi wa kata hiyo kuwa kituo hicho kilikamilika muda mrefu na kuna vifaa vyenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 160 vilipelekwa lakini havijafungwa kutokana na kukosekana kwa umeme.

Alisema atafanya ziara nyingine baada ya muda aliotoa kuisha ili kujiridhisha kama agizo hilo litakuwa limetekelezwa na kwamba kama halitakuwa limetekelezwa wahusika watachukuliwa hatua kali.

"Hiki kituo kina hadhi ya kuwa Hospitali ya Wilaya. Katika nchi hii vituo vingi vilivyojengwa vimekuwa vikigharimu sio zaidi ya Sh. milioni 500, lakini hiki kimegharimu fedha ambazo zingetosha hata vituo vitatu, sasa kukosekana kwa umeme ni tatizo kubwa sana," alisema Dk. Chuachua.

Alisema ili kuhakikisha vifaa vilivyohifadhiwa kwenye vituo hivyo Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya imeelekezwa kupeleka mlinzi mwenye weledi ili asaidiane na wananchi kuvilinda.

Hata hivyo alimwagiza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Steven Katemba, kuanza ujenzi wa nyumba za watumishi wa kituo hicho huku akiwataka wananchi pia kushiriki kwa kusaidia kusomba mawe na mchanga.

Awali, Njeza alisema Kituo cha Afya cha Ikukwa ni muhimu kwa wananchi wa kata hiyo pamoja na kata za jirani za wilaya za Chunya na Songwe.

Alisema alianza kuwasaidia wananchi hao kwa kuwapelekea umeme wa jua katika iliyokuwa zahanati ya Kijiji cha Ikukwa baada ya kubaini kuwa manesi walikuwa wanatumia vijinga vya moto kuwazalisha wanawake.

Alisema alitoa msaada huo akiwa bado si mbunge, lakini baada ya kuwa mbunge aliwekeza nguvu kubwa ili kuhakikisha wananchi hao wanajengewa kituo cha afya.

"Kwa sasa serikali inaendelea na utekelezaji wa mradi wa umeme vijijini kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA) na hapa tayari nguzo zimewekwa lakini tunaomba kasi iongezeke ili kituo chetu hiki kiunganishiwe umeme ili wananchi waendelee kupata huduma," alisema Njeza.

Alisema kwa sasa wananchi wa kata hiyo wanalazimika kusafiri umbali wa zaidi ya kilomita 70 kwenda kutibiwa katika Hospitali Teule ya Wilaya ya Ifisi iliyoko katika Mji Mdogo wa Mbalizi hali ambayo alisema ni hatari hasa kwa wajawazito.

Msimamizi wa Miradi ya REA wa TANESCO Mkoa wa Mbeya, Anacletus Magembe, alisema watahakikisha mpaka kufikia Desemba umeme utakuwa umeshaunganishwa kwenye kituo hicho pamoja na taasisi mbalimbali za umma katika kata hiyo.



Mbunge wa Mbeya Vijijini, Oran Njeza, akizungumza na wananchi wa Kata ya Ikukwa katika Halmashauri ya Mbeya juzi, alipofanya mkutano wa hadhara baada ya kukagua miradi ya maendeleo. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Wajasiriamali watakiwa kurasmisha biashara zao

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAJASIRIAMALI wa mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, wameshauriwa kurasmisha biashara zao ili wanufaike na soko huru la Afrika Mashariki ambalo liliridhiwa na Bunge kwenye vikao vyake vya hivi karibuni.

Ushauri huo ulitolewa juzi na Katibu Tawala Msaidizi Uchumi na Uzalishaji wa Mkoa wa Mbeya, Said Madito, alipokuwa anafungua Kongamano la Biashara kwa Wajasiriamali wa Nyanda za Juu Kusini lililofanyika jijini hapa.

Kongamano hilo liliandaliwa na Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF) kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara na kushirikisha zaidi ya wajasiriamali 100 kutoka katika mikoa yote ya ukanda huo.

Madito alisema Soko Huru la Afrika Mashariki litakuwa na manufaa kwa wajasiriamali wote endapo watajiwekea utaratibu mzuri wa kurasimisha biashara zao na kuhifadhiwa vizuri.

"Bidhaa zetu zinakuwa si za ushindani kwa sababu nyingi hazijarasimishwa na hata vifungashio vyetu havina ubora unaowezesha bidhaa hizi kuwa za ushindani, sasa nawashauri wajasiriamali mchangamke," alisema Madito.

Alisema serikali kwa sasa inahimiza uchumi wa viwanda na imeweka mazingira mazuri ya watu kuwekeza kwenye sekta hiyo, lakini tatizo lililopo kwa sasa ni wajasiriamali wadogo kutozalisha bidhaa zenye ubora mzuri.

Baadhi ya wafanyabiashara walioshiriki kongamano hilo walisema wako tayari kuchangamkia soko la Afrika Mashariki na watahakikisha wanafanya biashara kiushindani na mataifa mengine ya ukanda huo.

# Naibu waziri ataka kasi mashauri ya watoto

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

NAIBU Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, Mwanaidi Ally Khamis, ameagiza maofisa maendeleo ya jamii nchini kwa kushirikiana na watumishi wa mahakama za watoto kushughulikia haraka mashauri ya watoto wanaokinzana na sheria ili kuepusha jamii kuyamaliza kienyeji.

Aliyasema hayo juzi jijini hapa alipotembelea Mahakama ya Watoto ya Mkoa wa Mbeya. Alisema kitendo cha kuchelewa kushughulikia mashauri hayo kinasababisha watoto kukosa haki zao za msingi.

Pia alisema umekuwapo utaratibu wa watoto kuwekwa mahabusu wakituhumiwa kwa makosa mbalimbali, lakini kesi zao zinakaa muda mrefu bila kushughulikiwa na zinakuja kuanza kushughulikiwa wakiwa tayari wamefikisha umri wa utu uzima.

Aliwataka watumishi hao kuhakikisha wanaweka maslahi ya watoto mbele wakati wa kushughulikia mashauri hayo kwa maelezo kuwa kundi hilo ni miongoni mwa makundi maalumu ambayo yanatakiwa kuhudumiwa kwa weledi.

"Mtoto anaweza akawa amefanyiwa ukatili kwenye jamii pengine amebakwa, sasa kesi inapocheleweshwa mnasababisha mianya ya wazazi kuanza kujadiliana huko nyumbani na kukubaliana. Wakishafikia hatua hiyo ndio kesi inaanza kuyeyuka na mtoto anakosa haki yake," alisema Mwanaidi.

Kaimu Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Watoto wa Mkoa wa Mbeya, Zawadi Laizer, alisema tatizo la kuchelewa kusikilizwa kwa mashauri yanayowahusu watoto huwa linasababishwa na ucheleweshwaji wa upelelezi.

Alisema mahakama huwa inasubiri mpaka upelelezi wa shauri lolote ukamilike hasa kwa mashauri yanayohusu masuala ya jinai na kwamba wao kama mahakama huwa hawawezi kuendesha kesi kabla upelelezi haujakamilika.

Hakimu Laizer alisema baadhi ya watoto huwa wanakabiliwa na mashtaka makubwa yakiwamo ya mauaji jambo ambalo huwa linahitaji ushahidi wa kutosha na hivyo wakati mwingine upelelezi huwa unachukua muda mrefu kukamilika.

"Upelelezi ukikamilika mapema hata usikilizwaji wa mashauri siyo ya watoto tu bali hata ya watu wazima huwa nao unaharakishwa lakini ikiwa kinyume chake ndiyo haya ambayo Naibu Waziri anayasema," alisma.

Baadhi ya maofisa ustawi wa jamii waliiomba serikali kuwapatia mafunzo ya mara kwa mara ili wawe na uelewa mzuri kuhusu mashauri ya watoto pamoja na makundi mengine maalumu ambayo yanawahusu.

Mmoja wa maofisa hao, Shangwe Mshana, alisema baadhi ya maofisa ustawi wa jamii wanakuwa wageni kazini na hawana uelewa wa kutosha kuhusu mashauri ya watoto hali ambayo wakati mwingine huwa inawasababishia kutokuwa na weledi wa kutosha.

Pia aliomba baadhi ya sheria zirekebishwe kutokana na kuwa na masharti ambayo yanawanyima watoto haki zao akidai kuwa huwa zinalazimisha mtoto akifanya kosa asubiri mpaka afikishe umri wa miaka 18 ndipo kesi yake ianze kusikilizwa.

Akiwa mkoani Mbeya, Naibu Waziri Mwanaidi alitembelea pia Chuo cha Maendeleo ya Jamii cha Uyole jijini Mbeya ambako aliweka jiwe la msingi la ujenzi wa darasa na kisha akatembelea Shule ya Madilisho ya Ilambo.





# Mufti amfungia mwalimu anayedaiwa kudhalilisha

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

OFISI ya Mufti Mkuu wa Zanzibar imemfungia kutofanya kazi za kusomesha mwalimu wa madrasa, Ali Abdalla Ali, anayetuhumiwa kwa makosa ya udhalilishaji dhidi ya wanafunzi wake.

Akizungumza jana na waandishi wa habari mjini Zanzibar, Katibu wa Mufti Mkuu wa Zanzibar, Sheikh Khalid Mfaume, alisema uamuzi huo umechukuliwa kwa kuwa tuhuma zinazomkabili zinaonyesha amekiuka maadili ya kazi ya kusomesha kwa kuwadhalilisha wanafunzi na hivyo ameondolewa katika orodha ya usajili wa walimu wa madrasa.

Alisema vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia kwa wanafunzi havikubaliki na vinakwenda kinyume cha maadili ya kazi ya ualimu ambayo ni kuonyesha njia na kusomesha wanafunzi.

Sheikh Mfaume alisema Ofisi ya Mufti imemfungia mwalimu huyo kutofundisha sehemu yoyote pamoja na kuifungia madrasa yake na kuwataka wazazi kuwaondoa wanafunzi wote katika madrasa hiyo na kuwatafutia madrasa nyingine.

"Ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar imeifungia madrasa ya Bismillahi kuendelea kutoa elimu pamoja na kupokea walimu ambapo pia mwalimu anayetuhumiwa na kesi ya udhalilishaji haruhusiwi kufanya kazi ya kusomesha katika madrasa yoyote nchini," alisema.

Aliongeza kuwa Ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar imeanza usajili wa vyuo vya madrasa vyote vilivyopo nchini kwa lengo la kutambua idadi yake na kuhakiki walimu wote.

Alisema kwa mujibu wa sheria, vyuo vyote vinatakiwa kusajiliwa na kuhakikiwa walimu wake, hatua ambayo itasaidia kupambana na matukio ya udhalilishaji wa kijinsia.

"Ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar tunaendelea na kazi ya kusajili vyuo vya madrasa pamoja na walimu wake kwa ujumla, hatua ambayo itatusaidia kujua mwelekeo wa vyuo hivyo na kupambana na vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Magharibi A Unguja, Suzan Kunambi, aliitaka Ofisi ya Mufti kuchukua hatua kwa madrasa ambazo zitabainika walimu wake kujihusisha na vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia.

Alisema matukio ya vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia dhidi ya wanafunzi hayakubaliki, akisisitiza walimu wanatakiwa kuwa kioo cha jamii katika kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa sheria na taaluma ya kazi zao.

Mwalimu huyo wa madrasa anashikiliwa na Jeshi la Polisi kwa tuhuma za kuwadhalilisha na kulawiti wanafunzi wake watano.

Matukio ya udhalilishaji yameendelea kuripotiwa visiwani Zanzibar licha ya Rais Dk. Hussein Mwinyi kutangaza dhamira yake ya kukabiliana nayo kwa kuanzisha mahakama maalum ya kupambana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia.



Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Simai Mohammed Said (wapili kushoto) na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako (kushoto), wakiangalia madhara yaliyotokana na kuungua moto kwa jengo la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam Sayansi za Bahari, Forodhani Mjini Unguja. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Walimu wapewa mbinu tija za uchumi wa bluu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKURUGENZI Mtendaji wa Mamlaka ya Mafunzo ya Amali Zanzibar, Bakari Ali Silima, amewataka walimu kuzifahamu fursa zilizopo katika uchumi wa bluu, ili kuwaelekeza vijana kufikia lengo la ukuaji wa uchumi nchini.

Alisema taifa lolote linalotaka kuendelea, elimu ni nguzo muhimu katika ukuaji wa uchumi na kufikia malengo yaliyopangwa.

Akizungumza juzi katika maadhimisho ya Siku ya Walimu Duniani huko Chuo Kikuu cha Taifa Suza Kampasi ya Utalii, alisema walimu wanapaswa kujua fursa zilizopo nchini hasa kupitia uchumi wa bluu pamoja na kuongeza nguvu kubwa katika utoaji wa taaluma zao.

Mkurugenzi huyo aliwataka vijana kuwa makini katika kuchangamkia fursa zinazotolewa na walimu hao ili kufikia malengo yao waliojiwekea.

Akiwasilisha mada ya historia ya walimu, Mwalimu Daudi Ali kutoka Chama cha Walimu Zanzibar, alisema walimu wanapaswa kuthaminiwa katika jamii kutokana na msaada wanaotoa katika kuwaelimisha vijana nchini kwa kuwapatia taaluma bora.

Hata hivyo, mwalimu huyo alikuwa na angalizo kwamba bado kuna baadhi ya walimu ambao wana mtazamo finyu juu ya wanafunzi wenye mahitaji maalum.

Alisema vikwazo vinavyowakabili walimu ni pamoja na kutopata mafunzo ya elimu mjumuisho katika shule zao, jambo ambalo linaleta usumbufu katika ufundishaji kwa watu wenye ulemavu.

## Waziri ahimiza mkakati kuinua wenye ulemavu

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Dk. Saada Mkuya Salum, amezishauri taasisi za serikali na binafsi zinazotoa huduma kwa jamii kutoa kipaumbele kwa watu wenye mazingira maalum wakiwamo watu wenye ulemavu wa kusikia.

Dk. Saada aliyasema hayo jana wakati akiyafungua mafunzo maalum ya lugha ya alama kwa watendaji wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF) yaliyoandaliwa na Baraza la Taifa la Watu Wenye Ulemavu kwenye Ukumbi wa ZSSF, Kariakoo mjini Zanzibar.

Aliipongeza ZSSF kwa kuwa mfano bora kwa mashirika ya serikali kuonyesha kwa vitendo na dhamira njema ya kuwahudumia wananchi wa makundi yote kwa kuanza na lugha ya alama ambayo itawasaidia viziwi kupata huduma wanazozitoa kwa uhakika bila ya gharama ya kutafuta mkalimani.

Aliiomba ZSSF isiishie hapo bali kutafuta njia nyingine ya kuwasaidia watu wenye ulemavu wa uoni kwa kuangalia uwezekano wa kutengeneza kadi za ZSSF zenye alama ya nukta nundu.

"Ninaziomba taasisi za serikali ili tuwe na jamii shirikishi, hata vitabu vya sera na sheria na vinginevyo tuhakikishe tunaandika kwa nukta nundu ili wenzetu wenye ulemavu wa uoni nao wasome maendeleo ya nchi," alisema.

Alibainisha kuwa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kupitia Baraza la Watu Wenye Ulemavu inatambua kuwa fursa mpya ya uchumi wa bluu ni kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wote wa Zanzibar, hivyo imejipanga kuandaa mpango mkakati wa kuona lugha ya alama inapewa kipaumbele kufundishwa kwenye taasisi zote zinazotoa huduma kwa jamii.

Mkurugenzi wa Baraza la Watu Wenye Ulemavu, Ussy Khamis Debe, alisema mafunzo ya lugha ya alama yameanzishwa baada ya kuonekana kuna upungufu katika taarifa kwa watu wenye ulemavu wa usikivu.

Ussy alisema miongoni mwa vikwazo vinavyowapata watu wenye ulemavu wa usikivu ni kutopata taarifa sahihi na kwa wakati mwafaka na ndio maana baraza hilo likaamua kuendelea kutoa elimu hiyo ya lugha ya alama kwa taasisi mbalimbali.

Mafunzo kama hayo pia hutolewa na Jumuiya ya Wakalimani wa Lugha ya Alama (JUWALAZA), Chama cha Viziwi Zanzibar (CHAVIZA) na Chuo cha Taifa cha Zanzibar (SUZA).

## Wadau: Kibiti inatisha ukatili dhidi ya watoto

**Na Halfani Chusi**

WADAU kutoka asasi zisizo za kiserikali (NGO) wamebaini kuwapo kwa madhila mengi kwa mtoto wa kike wilayani Kibiti mkoani Pwani ikiwamo mimba za utotoni, ukosefu wa taulo za kike na ajira tumikishi.

Walibainisha hayo juzi mkoani Dar es Salaam wakati wa hafla ya uzinduzi maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Kike Afrika. Kilele cha maadhimisho hayo kinatarajiwa kufanyika wilayani Kibiti Oktoba 11 mwaka huu.

Akizungumza katika hafla hiyo, Julieth Sewawa, ambaye ni mhitimu wa kidato cha sita, alisema lengo na maadhimisho hayo ni kutoa elimu katika wilaya nne za Mkoa wa Pwani.

Julieth alisema elimu hiyo itasaidia kuvunja pengo la kijinsia kati ya wavulana na wasichana katika nyanja zinazohitaji teknolojia ya kisasa.

Alisema uwakilishi wa wanawake unapokuwa mdogo katika suala la teknolojia unaweza kusababisha uchumi wa nchi kushuka.

Julieth aligusia historia ya maisha yake, akibainisha namna alivyopambana hadi kufikia malengo na kuwaomba watoto wengine wa kike kuiga mfano huo.

"Nina umri wa miaka 20 ni muhitimu wa kidato cha sita, ni msichana wa kisasa, ninapenda sana teknolojia tokea nilipokuwa mdogo, nilikuwa nikiona kompyuta mikono yangu ilikuwa inawasha na kutamani kuichezea, baada ya hapo nikajiunga na shule ya upili Jangwani na huko nikasoma masomo ya sayansi na kompyuta.

"Baada ya hapo nikajiunga na klabu iliyokuwa inasimamiwa na Shirika la Absen Girls, ambapo tulifundishwa vitu mbalimbali ikiwamo kutengeneza programu za kompyuta.

"Baada ya hapo nikapata nafasi ya kushiriki katika mashindano ya First Interpreneurship Sernit' mimi na timu yangu tulifanikiwa kuwa washindi wa pili. Hapo ndipo nilizidi kupata nguvu na baada ya hapo pia nilifanikiwa kutengeneza programu kwenye simu ya kuwezesha kugundua dawa feki na nzima kabla ya kizitumia," alisema.

Aliomba wadau mbalimbali na serikali kulipa kipaumbele kundi la watu wenye ulemavu katika masuala ya teknolojia.

Mratibu wa kitaifa kupinga ajira kwa mtoto wa kike, Scolastika Pembe, alitoa wito kwa wadau wengine kushirikiana nao kuelekea kilele cha maadhimisho hayo.

Mratibu Msaidizi, Radhia Mallah, aliishukuru TCACL na Taasisi ya Jakaya Mrisho Kikwete kwa kufanikisha uzinduzi wa shughuli hiyo maalum.

# Serikali yaongeza juhudi uwekezaji miradi kimkakati

**Na Mwandishi Maalumu**

SERIKALI imenunua shamba la Mngeta lenye ukubwa wa hekta 5,818 lililoko Kilombero mkoani Morogoro kutoka kwa mfilisi aliyewekwa na Benki ya NMB baada ya mwekezaji kushindwa kuliendesha.

Shamba hilo limenunuliwa ikiwa ni sehemu ya juhudi za kuhakikisha serikali inawezekeza katika miradi ya kimkakati, ikiwamo ya sekta ya kilimo.

Ununuzi wa shamba hilo umefanyika baada ya serikali kulinunua kwa Mfilisi, Silvanus Mlola, aliyewekwa na Benki ya NMB ambaye ni Mdai wa Kampuni ya Kilombero Plantation Limited, baada ya kushindwa kujiendesha na kulipa madeni ya mikopo.

Akizungumza wakati wa kutiwa saini kwa makabidhiano ya hati na nyaraka mbalimbali za umiliki wa shamba hilo yaliyofanyika juzi katika Ofisi ya Msajili wa Hazina jijini Dar es Salaam, Msajili wa Hazina, Mgonya Benedicto, alisema serikali imeamua kununua shamba hilo kutokana na umuhimu wake kwa taifa.

Benedicto alisema hatua hiyo imezingatia eneo lilipo shamba hilo na malengo ya serikali ya maendeleo endelevu. Alisema shamba la Mngeta liko katika eneo la kimkakati kwa kilimo na kwamba litaleta manufaa makubwa ya kiuchumi kwa wananchi wanaolizunguka eneo hilo.

Kampuni ya Kilombero Plantation Limited iliwekwa chini ya mfilisi baada ya menejimenti ya kampuni hiyo kushindwa kuendesha shamba kwa faida na kusababisha hasara na madeni yasiyolipika katika kipindi chote cha makubaliano, hivyo kushindwa kufikia matarajio na makubaliano yaliyofanywa na serikali wakati wa ubia wa kibiashara.

Kuhusu malengo ya awali ya uanzishwaji wa shamba la Mngeta, Msajili wa Hazina alisema shamba hilo lilikusudiwa kuwekewa miundombinu ya umwagiliaji ili kuzalisha mazao ya chakula kwa lengo la kujitosheleza kwa chakula nchini, malengo ambayo hayakufikiwa kama ilivyotarajiwa na hivyo kuingiza katika mazingira ya Serikali kupoteza umiliki wake.

Naye Mfilisi wa shamba hilo, Mlola aliishukuru serikali kwa ushirikiano na kukamilisha kwa wakati makubaliano yote yaliyofikiwa katika suala hilo.




Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Arusha, Suleiman Msumi akizungumza wakati akizindua duka la Vodacom pamoja na wiki ya huduma kwa wateja, jijini Arusha jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mhagama aipa kibarua bodi WCF

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, ameitaka Bodi ya Wadhamini ya Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) kusimamia maslahi ya wafanyakazi yanayotokana na kuanzishwa kwa sheria ya mfuko huo.

Mhagama alitoa agizo hilo jana wakati akizindua Bodi ya Mfuko huo katika hafla iliyofanyika mjini hapa.

Waziri Mhagama aliwataka wajumbe wa bodi kuyaelewa vyema majukumu yao kama yalivyoanishwa kisheria na sehemu ya majukumu hayo ni pamoja na kusimamia maslahi ya wafanyakazi kwa kufuata sheria.

Alimpongeza Mwenyekiti Mpya wa Bodi hiyo , Emmanuel Humba, kwa kuaminiwa na Rais wa Samia Suluhu Hassan kushika wadhifa pamoja na wajumbe wa bodi aliowateua na kuwataka waende kuusimamia mfuko kwa kushirikiana na menejimenti ili kufikia matarajio ya serikali.

Wajumbe wapya wa Bodi waliloteuliwa ni pamoja na Onorius Njole, Perfect Kilenzi, Ibrahim Mahuni, Abdulaziz Shambe, Rifai Mkumba, Julian Mpanduji, Rehema Ludanga na Felix Rugarabamu.

"Tunapofanya maamuzi (uamuzi) haya (huu) mazito (mzito) ya (wa) kuwateua, tunajua bodi ni chombo cha juu cha uendeshaji wa kila siku wa taasisi husika. Sisi sote hata Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko, wafanyakazi wenyewe, waajiri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Rais ni kama vile tumekasimu madaraka yetu kwa mujibu wa sheria na kukasimu kwako mwenyekiti na bodi," alisema.

Waziri huyo alisema mfuko huo umekuwa na maafanikio katika kipindi cha miaka sita, hivyo ana imani bodi hiyo itaendelea kuyalinda mafanikio hayo ili kuongeza tija.

Alisema moja ya mafanikio hayo ni pamoja na mfuko kukua hadi kufikia Sh. bilioni 445.49 kutoka thamani ya mfuko mwaka 2016/2017 ambao ulikuwa Sh. bilioni 112.83.

Kuhusu ulipaji wa mafao, Waziri Mhagama alisema hadi kufikia 2020/21 mfuko ulilipa mafao ya wafanyakazi waliopata ajali kazini yenye thamani ya Sh. bilioni 12.43 ikilinganishwa na mwaka 2017 ambapo zililipwa Sh. bilioni 1.55 tu.

Mwenyekiti wa Bodi, Humba, alimhakikishia Waziri Mhagama kuwa watahakikisha wanaendelea kutekeleza majukumu kulingana na malengo ya mfuko.

"Yapo mashirika mengi yanakufa kutokana na kujisahau kwa waliopewa dhamana ya kusimamia mashirika haya. Sisi ni wadhamini tu kwa hiyo udhamini wetu lazima tuulinde kwa hali na mali kwa kutenda haki," alisema Humba.

Hata hivyo Mwenyekiti huyo alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kumuamini kuongoza Bodi hiyo na kutoa hakikisho ya kufanya kazi kwa uwezo wake wote.

Awali, Mkurugenzi Mkuu wa WCF, Dk. John Mduma, alimpongeza Humba kwa kuaminiwa kupewa dhamana hiyo kwa kipindi cha pili huku akiwapongeza wajumbe wote walioteuliwa na waziri katika kuendesha gurudumu la mfuko.

HABARI MICHEZO

# TWIGA STARS, ZAMBIA MAJARIBUNI COSAFA

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Soka ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars), inatarajia kuwavaa Zambia (She-polopolo) katika mechi ya hatua ya nusu fainali ya mashindano ya Kombe la COSAFA itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Wolfson ulioko Port Elizabeth nchini Afrika Kusini.

Mechi hiyo inatarajiwa kuwa ngumu kutokana na timu zote kushinda mechi zake tatu za hatua ya makundi.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Twiga Stars, Bakari Shime alisema timu yake imejiandaa vyema kuelekea mchezo huo kwa sababu wanaamini utakuwa mgumu na wenye ushindani wakati wote.

Shime alisema timu zote zinazoshiriki michuano hiyo mwaka huu zimejiandaa na kuongeza malengo ya Twiga Stars ni kutinga fainali ya michuano hiyo.

"Zambia ni timu nzuri na siku zote wamekuwa ni wapinzani wetu sana, lakini tumejiandaa kukabiliana nao kwa sababu tangu mwanzo tulijua kama hatukucheza na Uganda, basi tutacheza na Zambia ambayo ilikuwa Kundi C," alisema Shime.

Twiga Stars ilimaliza kinara katika Kundi B, baada ya kupata ushindi mnono katika mechi zote tatu walizocheza.

Wawakilishi hao wa Tanzania walianza michuano hiyo kwa kuwachapa Zimbabwe mabao 3-0, halafu wakashinda tena magoli 2-0 dhidi ya Botswana na walimaliza hatua hiyo ya makundi kwa ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Sudani Kusini.

Wakati kanuni ya michuano hiyo, ikiruhusu kuzikutanisha timu zote zilizoongoza makundi B na C, mechi nyingine ya hatua ya nusu fainali itakayochezwa leo kati ya wenyeji Afrika Kusini (Banyana Banyana), dhidi ya Malawi.

Banyana Banyana walimaliza hatua ya makundi wakiwa na pointi saba wakati Malawi yenyewe ilishinda mechi mbili za hatua hiyo ya awali.

Fainali ya mashindano hayo yanayochezwa kila mwaka itafanyika keshokutwa Jumamosi.



Vijana wa hamasa wakitoa burudani wakati wa mapokezi ya Mjumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Mlezi wa chama hicho Mkoa wa Dar es Salaam, Makamu wa Rais Dk. Philip Mpango ambaye alifanya ziara maalumu jijini juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# KMC yaipeleka Yanga Songea

**Na Faustine Feliciane**

KOCHA wa KMC , Habib Kondo, amesema uamuzi wa kuupeleka mchezo wao wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Yanga kwenye Uwanja wa Majimaji, Songea ni kwa ajili ya kusambaza burudani ya soka nchini na si kuwaondoa mjini wapinzani wao.

KMC itakuwa mwenyeji dhidi ya Yanga katika mchezo wa Ligi Kuu Bara utakaochezwa Oktoba 19, mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kondo alisema wamejiandaa na wanaendelea kujipanga imara kwa ajili ya kukabiliana na Yanga katika mchezo huo muhimu.

Kondo alisema wanafahamu Yanga itashuka dimbani ikiwa na rekodi ya kushinda michezo yake miwili iliyotangulia, lakini hilo hawalihofii.

"Ule uwanja wa Majimaji hata sisi sio wa kwetu, tunaenda kule kuwapelekea burudani watu wa kule, kiufundi bado tunaendelea kujipanga kwa ajili ya mchezo huo, hatuiogopi Yanga bali tunaiheshimu kama zilivyotimu nyingine za Ligi Kuu msimu huu," alisema Kondo.

Naye Walter Harrison, Ofisa Mkuu wa KMC aliongeza wamepeleka mchezo huo Songea kwa sababu ya kuwapa burudani watu wa huko.

KMC ina pointi moja baada ya kufungwa mechi moja na kutoka sare mchezo mwingine.

## Metacha aanza ligi kwa 'assist'

**Na Adam Fungamwango**

KATIKA hali isiyo ya kawaida, katika mechi 16 zilizochezwa za Ligi Kuu Tanzania Bara na 'kuzaa' mabao 22, magoli mawili yametokana na pasi za mwisho za makipa, Metacha Mnata wa Polisi Tanzania na Haroun Mandanda wa Mbeya City.

Nusura kipa wa Simba, Aishi Manula naye aingie kwenye rekodi hiyo kama mpira wake mrefu alioupiga golini kuelekea kwenye lango la Dodoma Jiji FC, usingeguswa na Chriss Mugalu, Ijumaa iliyopita Simba ikishinda bao 1-0, Jamhuri Dodoma, Ijumaa iliyopita.

Mandanda, yeye alipiga mpira mrefu kutoka golini ambao ulikwenda moja kwa moja kwenye kichwa cha Peter Mapunda akiwa amesimama katikati ya mabeki wawili wa Prisons, akaruka kidogo kuubadili uelekeo na kujaa wavuni.

Lilikuwa ni bao pekee lililofungwa kwenye dakika ya pili ya nyongeza na kuipatia Mbeya City ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Tanzania Prisons kwenye Uwanja wa Sokoine hapo Septemba 28, mwaka huu.

Metacha, aliyeachwa na Yanga, naye alifanya kama mwenzake kwenye mechi dhidi ya Azam FC, Uwanja wa Ushirika, Moshi mkoani Kilimanjaro, Jumamosi iliyopita. Jumla ya wachezaji 14 wametoa 'assist' kwenye Ligi Kuu mpaka sasa, Obrey Chirwa wa Azam FC na Paul Kasunda wa Mbeya Kwanza wakiongoza kwa kutoa pasi mbili za mabao kila mmoja mpaka sasa.

## Eritrea yawasili kuivaa Tanzanite

**Na Saada Akida**

KIKOSI cha Timu ya Soka ya vijana cha wasichana wa umri chini ya miaka 20 kutoka Eritrea kinatarajia kuwasili leo mchana kwa ajili ya mchezo wa marudiano dhidi ya wenyeji Tanzanite utakaochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa Azam Complex jijini Dar es Salaam.

Ofisa Habari na Mawasiliano wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Clifford Ndimbo aliliambia gazeti hili maandalizi kuelekea mchezo huo yamekamilika na wanaamini Tanzanite itapata matokeo mazuri.

Ndimbo alisema kikosi cha Tanzanite kimejiandaa kukamilisha 'kazi' waliyoifanya ugenini ili wasonge mbele kwenye michuano hiyo.

"Maandalizi yanaenda vyema, tunatarajia kuwapokea Eritrea kesho (leo), saa 7: 00 mchana, pia waamuzi wataingia jioni, tunatarajia wawakilishi wetu wataendelea kupeperusha vyema bendera ya nchi," Ndimbo alisema.

Tanzanite itashuka dimbani ikiwa na kumbukumbu ya ushindi wa mabao 3-0 walioupata ugenini jijini Asmara wiki iliyopita.

Mshindi wa jumla wa mechi hiyo ya kusaka tiketi ya kucheza fainali za vijana za Kombe la Dunia atakutana na Burundi au Namibia.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

### RUDIGER ATOA MSIMAMO

MLINZI wa Timu ya Taifa ya Ujerumani na Chelsea, Antonio Rudiger mwenye umri wa miaka 28, amesema hatetereshwi na tetesi zinazomhusisha yeye na Bayern Munich. **(Mirror)**

### TUCHEL AMTAKA RUDIGER

WAKATI mkataba wa Antonio Rudiger ukitarajiwa kumalizika kipindi cha majira ya joto yajayo, kocha wa Chelsea, Thomas Tuchel anatamani mlinzi huyo wa kati asaini mkataba mpya. **(Express)**

### PEREZ AMSUBIRI MBAPPE

RAIS wa Real Madrid, Florentino Perez ana matumaini mshambuliaji wa Paris St-Germain, Mfaransa Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 22 atajiunga na klabu hiyo mwaka 2022.**(El Debate)**

### VLAHOVIC MAMBO BADO

KLABU ya Fiorentina imesema mshambuliaji wake, Dusan Vlahovic ambaye ni raia wa Serbia mwenye umri wa miaka 21, anayehusishwa na kuhamia Arsenal na Tottenham, hajakubali mkataba mpya na klabu hiyo ya Serie A. **(Evening Standard)**

### BREMER ANUKIA LIVERPOOL

LIVERPOOL bado wana nia na mchezaji wa nafasi ya ulinzi wa Torino, Bremer mwenye umri wa miaka 24, lakini Manchester United na Manchester City zimekuwa pia zikimfuatilia Mbrazili huyo. **(Calciomercato via TEAMtalk)**

### ADEYEMI SOKONI RASMI

KLABU ya Red Bull Salzburg inahitaji kati ya pauni milioni 25 na milioni 34 kwa ajili ya kumwachia mshambuliaji wa Mjerumani, Karim Adeyemi, ambaye anatolewa macho na klabu ya Liverpool na Bayern Munich**. (Sky Germany)**

### JUVE KUMWACHA MCKENNIE

KLABU ya Juventus inajiandaa kuachana na kiungo wa kati wa raia wa Marekani, Weston McKennie, ambaye anatakiwa na Tottenham Hotspur na West Ham. **(TEAMtalk)**

### ONANA KUTUA INTER

GOLIKIPA wa Ajax na Timu ya Taifa ya Cameroon, Andre Onana mwenye umri wa miaka 25, yuko tayari kujiunga na Inter Milan kama mchezaji huru ifikapo mwaka 2022. **(Fabrizio Romano)**

### XAVI, BARCA WATETA

BARCELONA imeendelea na mazungumzo na kiungo wa kati wa zamani, Xavi mwenye umri wa miaka 41 ili achukue nafasi ya kocha, Ronald Koeman, lakini makubaliano na raia huyo wa Hispania hayajafikiwa. **(90min)**

### LENO NAMBA MBILI

BENO Leno mwenye umri wa miaka 29, yuko hatarini kuwa chaguo la pili la Ujerumani, ambalo litafanya kuondoka kwake Arsenal Januari kuwa jambo linalowezekana. **(Fussball.News, via Star)**

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# DEPAY: SIJUTII KUHAMIA BARCA

●●● Afunguka changamoto inayopitia klabu hiyo kwa sasa itamalizika na...

**BARCELONA, Hispania**

MEMPHIS Depay amesisitiza "kamwe hatajuta" kuhamia Barcelona licha ya klabu hiyo kuwa na mwanzo mgumu wa msimu huu.

Mshambuliaji huyo wa Uholanzi alihamia hapo Camp Nou kutoka Lyon kwa uhamisho huru, lakini hakupata nafasi ya kucheza pamoja Lionel Messi, ambaye aliondoka klabuni hapo kutokana na matatizo ya kifedha.

Kuondoka kwa raia huyo wa Argentina, kumeifanya Barcelona kuwa kwenye wakati mgumu, ikifungwa mechi zote mbili za mwanzo za makundi za Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa mabao 3-0, ikiwa inashika mkia katika kundi na imeshinda mechi tatu tu kati ya saba za LaLiga.

Hata hivyo, Depay anajivunia kuwachezea miamba hao wa Katalunya licha ya kuwa kwenye kiwango kibovu hivi sasa.

"Unaweza kuuliza (kama najutia kuhamia Barcelona)? Hii ni Barcelona. Sidhani kama unaelewa namna gani klabu kubwa zilivyo na nini maana yake mchezaji kucheza hapa. Kamwe sitajutia hilo," alisema Depay.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 alibainisha, Blaugrana hao wana nafasi ya kurudi kwenye kiwango chao licha ya sasa kuwa kwenye presha kubwa chini ya kocha, Ronald Koeman.

"Licha ya matokeo, nina furaha kubwa kuwa klabuni hapa," alisema Depay.

"Huu ni wakati mgumu kwa timu. Sitaki kuzungumza sana, lakini watu wanaongea kama vile msimu tayari umemalizika.

"Kuna mechi nyingi sana za kucheza. Bado kila kitu kipo wazi. Lakini kama mchezaji najihisi kuhusika na matokeo na natakiwa kuchukua majukumu yangu.

"Lazima ujali. Kila mchezaji anachukua jukumu lake hapa Barca. Hii ni kawaida kwa klabu kubwa kama Barcelona.

"Tunajua hali jinsi ilivyo kwa sasa. Tunajua kwamba ni ngumu. Tuna wachezaji wengi vijana na majeruhi wengi. Lakini nafikiri ni suala la muda tu mambo yatakuwa sawa."

MECHI KALI
HOME
AWAY
TANZANIA
2.44 | 2.87 | 2.97
BENIN
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom
m-pesa
halopesa
airtel money
ZANTEL EZYPESA
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249
18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

CHEZA USHINDE
JACKPOT
TZS. 559



# RUDIGER ASEMA NI HESHIMA KUTAKIWA BAYERN MUNICH

**LONDON, England**

ANTONIO Rudiger anaona ni heshima kubwa kwake kuhusishwa na uhamisho wa kujiunga na Bayern Munich, lakini mlinzi huyo amesema kwa sasa amejikita zaidi kuhakikisha anakuwa katika kiwango bora pale Chelsea.

Mlinzi huyo wa kati amekuwa mchezaji muhimu kwa Blues hao tangu ujio wa Thomas Tuchel, akiwa amezidiwa na Cesar Azpilicueta pekee aliyecheza dakika 2,054 kwenye Ligi Kuu England chini ya kocha huyo raia wa Ujerumani.

Hakuna mchezaji wa Chelsea aliyeweza kukaba vizuri zaidi kuliko Rudiger akiwa na asilimia 71.88, ambaye pia alikuwa hana dakika za kutosha chini ya zama za kocha, Frank Lampard.

Hata hivyo, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 bado majaliwa yake ya muda mrefu hapo Stamford Bridge hayajulikani.

Mkataba wake wa sasa unamalizika mwishoni mwa msimu huu, hivyo kumeibuka uvumi anaweza kuondoka kama mchezaji huru.

Bayern Munich imekuwa moja ya klabu inayotajwa kuwania saini ya Rudiger, ambaye amezungumzia kuhusu uvumi huo wakati akiwa kwenye majukumu ya Timu ya Taifa ya Ujerumani.

"Ni heshima, lakini siwezi kuruhusu mimi mwenyewe uvumi huu uniweke kwenye wakati mbaya," alisema akiwaambia waandishi wa habari, Jumanne.

"Nina majukumu kwenye klabu na hilo kuonyesha kiwango changu bora. Lakini inaonyesha umefanya mazuri kwa kipindi cha miezi na miaka iliyopita."



# Madrid imeikosea heshima PSG, Mbappe – Leonardo

**PARIS, Ufaransa**

MKURUGENZI wa Paris Saint-Germain, Leonardo ameijia juu Real Madrid kwa "kuwakosea heshima" miamba hao wa Ligue 1 na Kylian Mbappe baada ya kutangaza hadharani kumwania nyota huyo wa Timu ya Taifa ya Ufaransa.

Mbappe ambaye mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu huu, alithibitisha mwishoni mwa wiki hii aliomba PSG kuondoka kabla ya kuanza kwa msimu huu, huku Rais wa Madrid, Florentino Perez akibainisha nyota huyo anaweza kujiunga na miamba hao wa LaLiga, Januari mwakani.

Wakati Perez akidai alinukuliwa vibaya, nyota wa Madrid, Karim Benzema alisema uhamisho wa Mbappe kutua hapo kwenye dimba la Santiago Bernabeu ni "suala la muda tu" wakati Kocha wa Los Blancos, Carlo Ancelotti akiwaambia waandishi wa habari Mbappe "atafurahia mwenyewe" akiwa kwenye mji mkuu huo wa Hispania.

Leonardo amekasirishwa na taarifa hizo za Madrid kuhusu kuweka wazi mpango wa kutaka kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22.

"Huu ni mfano mmoja wapo wa kukosa heshima kwa PSG na Mbappe," alisema Leonardo katika mahojiano na L'Equipe.

"Kiukweli, wiki hiyo hiyo mchezaji wa Real Madrid, Karim Benzema, halafu Kocha wa Real Madrid, (Carlo Ancelotti).

"Na sasa ni rais, (Florentino Perez) anazungumza kuhusu Kylian kama vile tayari ni mchezaji wao. Narudia hii ni kukosa heshima, hatuwezi kuvumilia hili."

9,183,880

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 09/10/21 | 17:00 | Lugo vs Girona | 2.95 | 2.95 | 2.51 |
| 02. 09/10/21 | 17:00 | Hartlepool vs Northampton | 2.55 | 2.99 | 2.84 |
| 03. 09/10/21 | 17:00 | Bristol Rovers vs Carlisle | 2.55 | 3.09 | 2.75 |
| 04. 09/10/21 | 17:00 | Stevenage vs Exeter | 2.69 | 2.98 | 2.69 |
| 05. 09/10/21 | 17:00 | Sutton United vs Port Vale | 2.50 | 3.09 | 2.80 |
| 06. 09/10/21 | 17:00 | Barrow vs Leyton Orient | 2.55 | 3.14 | 2.70 |
| 07. 09/10/21 | 17:00 | Newport vs Bradford City | 2.79 | 3.19 | 2.45 |
| 08. 09/10/21 | 17:00 | Boreham Wood vs Dagenham and Redbridge | 2.49 | 3.22 | 2.68 |
| 09. 09/10/21 | 22:00 | Real Oviedo vs Sporting Gijon | 2.70 | 2.94 | 2.75 |
| 10. 10/10/21 | 08:00 | Matsumoto Yamaga vs Tochigi SC | 2.61 | 2.86 | 2.76 |
| 11. 10/10/21 | 15:00 | Real Sociedad B vs Ponferradina | 2.56 | 3.00 | 2.85 |
| 12. 10/10/21 | 19:15 | Alcorcon vs Burgos | 2.57 | 3.02 | 2.82 |
| 13. 10/10/21 | 22:00 | Fuenlabrada vs Leganes | 2.63 | 2.88 | 2.88 |

MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

ALHAMISI - 07 - OKTOBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:15 | 5387 | Hirnik-Sport vs FC Metalist Kharkiv | 9.50 | 5.43 | 1.24 |
| 14:00 | 3230 | South Korea vs Syrian Arab Republic | 1.27 | 4.66 | 10.67 |
| 14:00 | 3840 | Suphanburi vs Ratchaburi | 2.33 | 3.47 | 2.65 |
| 14:00 | 5310 | Latvia U21 vs San Marino U21 | 1.04 | 9.68 | 38.71 |
| 15:00 | 3056 | Chiangmai United vs Port FC | 3.63 | 3.63 | 1.84 |
| 15:30 | 1374 | Agrobiznes Volochisk vs FC Uzhhorod | 1.60 | 3.57 | 5.22 |
| 15:30 | 5190 | FC Podillya Khmelnytskyi vs Alliance Lypova Dolyna | 4.25 | 3.48 | 1.75 |
| 16:00 | 2221 | Tanzania vs Benin | 2.44 | 2.87 | 2.97 |
| 16:00 | 2830 | Faroe Islands U21 vs Macedonia U21 | 5.24 | 4.27 | 1.49 |
| 16:00 | 3223 | Liberia vs Cape Verde | 3.81 | 2.99 | 2.01 |
| 16:30 | 2175 | Vyskov vs Zlin | 4.64 | 4.35 | 1.54 |
| 17:00 | 5269 | AS Tel Aviv University W vs MS Kiryat Gat W | 3.53 | 4.06 | 1.77 |
| 17:00 | 5319 | Armenia U21 vs Serbia U21 | 8.93 | 5.24 | 1.26 |
| 17:30 | 1150 | Iraq vs Lebanon | 1.61 | 3.47 | 5.40 |
| 19:00 | 1075 | Rwanda vs Uganda | 2.91 | 2.66 | 2.66 |
| 19:00 | 4050 | Lillestrom SK 2 vs Ullensaker/Kisa 2 | 1.20 | 6.95 | 8.68 |
| 19:00 | 4995 | Nigeria vs Central African Republic | 1.10 | 7.54 | 18.36 |
| 19:00 | 5333 | Equatorial Guinea vs Zambia | 2.97 | 2.82 | 2.48 |
| 19:15 | 2278 | Germany U21 vs Israel U21 | 1.16 | 6.41 | 13.59 |
| 19:45 | 2211 | United Arab Emirates vs Iran | 3.69 | 2.86 | 2.11 |
| 19:45 | 5360 | Hapoel Raanana W vs Maccabi Kishronot Hadera W | 1.93 | 4.10 | 3.30 |
| 20:00 | 1215 | Aalesund 2 vs Volda | 1.50 | 4.75 | 4.56 |
| 20:00 | 1315 | China vs Vietnam | 1.73 | 3.49 | 4.36 |
| 20:00 | 3121 | Hapoel Beer Sheva W vs Bnot Netanya W | 3.97 | 4.36 | 1.63 |
| 20:00 | 4620 | Kosovo U21 vs Czech Republic U21 | 6.02 | 3.98 | 1.48 |
| 20:00 | 4805 | Saudi Arabia vs Japan | 3.30 | 2.91 | 2.23 |
| 20:00 | 5654 | Albania U21 vs Andorra U21 | 1.14 | 7.16 | 12.58 |
| 20:30 | 1031 | Bor. Freialdenhoven vs SV 1910 Breinig | 1.07 | 9.27 | 18.35 |
| 20:30 | 3276 | SV 1914 Eilendorf vs Viktoria Arnoldsweiler | 6.58 | 5.03 | 1.34 |
| 20:30 | 4103 | Fortuna Koln II vs SV Deutz 05 | 2.09 | 4.06 | 2.71 |
| 21:00 | 3891 | Turk Gucu Friedberg vs VfB Ginsheim | 1.47 | 4.66 | 5.05 |
| 21:05 | 4522 | Scotland U21 vs Denmark U21 | 2.80 | 3.35 | 2.45 |
| 21:15 | 2303 | Slovenia U21 vs England U21 | 6.94 | 4.43 | 1.38 |
| 21:30 | 3746 | Australia vs Oman | 1.42 | 4.16 | 6.58 |
| 21:45 | 2955 | Belgium vs France | 2.95 | 3.15 | 2.54 |
| 22:00 | 3429 | Mali vs Kenya | 1.59 | 3.48 | 5.61 |
| 22:00 | 4960 | Tunisia vs Mauritania | 1.17 | 6.61 | 11.66 |

IJUMAA - 08 - OKTOBA 2021

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 00:30 | 1397 | Sao Paulo vs Santos | 1.94 | 3.00 | 4.07 |
| 01:00 | 1741 | CD Tapatio vs Cancun FC | 2.46 | 3.14 | 2.70 |
| 02:00 | 3060 | Uruguay vs Colombia | 2.04 | 3.15 | 3.95 |
| 02:00 | 3333 | Paraguay vs Argentina | 5.99 | 3.54 | 1.64 |
| 02:30 | 3021 | Venezuela vs Brazil | 9.42 | 5.21 | 1.31 |
| 02:30 | 5701 | USA vs Jamaica | 1.27 | 5.05 | 8.94 |
| 03:05 | 4092 | Honduras vs Costa Rica | 2.51 | 2.85 | 2.90 |
| 03:30 | 4466 | Ecuador vs Bolivia | 1.15 | 7.23 | 18.07 |
| 04:00 | 1867 | Peru vs Chile | 2.64 | 3.04 | 2.84 |
| 04:40 | 4223 | Mexico vs Canada | 1.53 | 3.82 | 5.61 |
| 05:05 | 4592 | EL Salvador vs Panama | 3.15 | 2.76 | 2.40 |
| 16:00 | 5154 | Fastav Zlin B vs Sigma Olomouc B | 3.55 | 4.60 | 1.78 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# VLAHOVIC ATAKA KUJIUNGA JUVENTUS



**FLORENCE, Italia**

NYOTA wa Fiorentina, Dusan Vlahovic ana ndoto ya kuhamia Juventus, kwa mujibu wa Gazzetta dello Sport.

Uamuzi wa Vlahovic kukataa kuongeza mkataba wake na klabu hiyo ya Fiorentina kumesababisha vita kubwa, huku mchezaji huyo raia wa Serbia akiweka wazi anataka kuondoka.

Hata hivyo, Fiorentina wenyewe bado wana matumaini makubwa ya kumbakiza fowadi huyo ambaye yupo kwenye kiwango bora zaidi kwa sasa.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, mchezaji huyo ndoto yake kubwa ni kujiunga na miamba ya soka la Italia, Juventus, mara mkataba wake utakapomalizika mwishoni mwa msimu ujao.

Majaliwa ya Vlahovic yalianza kuwa kwenye shaka Fiorentina baada ya msimu uliopita kunukuliwa akisema anataka kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Mkataba wa sasa wa nyota huyo na Fiorentina utamalizika mwaka 2023 na Vlahovic mwenyewe yupo radhi kuondoka hata Januari mwakani.

Licha ya yeye mwenyewe kuitaka zaidi Juventus, lakini Manchester City, Tottenham Spurs, Atletico Madrid, Inter Milan na Arsenal pia zimekuwa zikiwania huduma ya nyota huyo.



# Lukaku atabiriwa kumzidi Ronaldo

**MANCHESTER, England**

NYOTA wa zamani wa Tottenham Hotspur, Darren Bent anaamini mshambuliaji wa Chelsea, Romelu Lukaku atafunga mabao mengi zaidi ya Cristiano Ronaldo wa Manchester United.

Lukaku mwenye miaka 28 amejiunga na Chelsea akitokea Inter Milan kwa mkwanja mrefu ambao ni pauni milioni 97.5, huku Ronaldo akiibukia United akitokea Juventus.

Dili la Ronaldo linatajwa kugharimu pauni milioni 15 ambazo mabosi wa United waliweka mezani kumpata nyota huyo mwenye miaka 36.

Msimu uliopita Ronaldo aliibuka mfungaji bora ndani ya Serie A ambapo alitupia mabao 29 na Lukaku yeye alikuwa namba moja katika timu yake ya Inter Milan ambapo alitupia magoli 24.

Nyota huyo amesema: "Nafikiria na kuiangalia Chelsea unaangalia mabao mengi yatapatikana kupitia Lukaku kwa sababu ndiyo mashine ambayo itakuwa mbele," alisema Bent akinukuliwa na Daily Mail.

"Tunafahamu ubora wa Ronaldo, lakini kuna Mason Greenwood, Bruno Fernandes, Rashford na Edinson Cavani, angalia sasa asicheze mechi zote tofauti na Lukaku yeye ana uhakika."

# Michezo

Alhamisi Oktoba 7, 2021

Nipashe





Depay: Sijutii kuhamia Barca

UKURASA 21




Rais wa Shirikisho la Soka Nchini (TFF), Wallace Karia (kulia), akiwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Taifa ya Biashara (NBC), Theobald Sabi, baada ya kutia saini mkataba na benki hiyo wa kudhamini Ligi Kuu Tanzania Bara katika hafla iliyofanyika jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Nabi ajipanga kuongeza 'dozi'

**Na Faustine Feliciane**

ILI kutimiza malengo ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu, Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi amesema kambi yao ya jijini Arusha italenga kupata 'dawa' ya tatizo la umaliziaji kwenye kikosi chake.

Nabi aliliambia gazeti hili jana hafurahishwi na namna timu yake inavyopoteza nafasi nyingi za kufunga na anataka kuona ligi itakaporejea baada ya kalenda ya kimataifa kumalizika, nyota wake wanakuwa tofauti.

Kocha huyo alisema timu yake ilistahili kupata ushindi mnono kwenye mechi zake mbili zilizopita, lakini hali ilikuwa tofauti na sasa anajipanga kumaliza tatizo hilo.

"Sijafurahishwa na namna washambuliaji wanavyokosa magoli ya wazi, nimeamua kulifanyia kazi suala hili mapema. Kambi ya Arusha nimeiomba ili nifanyie kazi mapungufu niliyoyaona kwenye timu yangu, tunatengeneza nafasi nyingi lakini kuzitumia kuna tatizo, ndio maana unaona tumeshinda goli moja katika kila mchezo," alisema Nabi.

Aliongeza bado anaimani na wachezaji wake kutokana na ubora wao na anaamini watakaporejea kwenye ligi kwa 'kishindo' kama walivyojiandaa.

"Ligi ni ngumu sana, kila timu imejipanga hivyo ni lazima kuwa makini hasa kutumia vyema kila nafasi tunayoitengeneza kwenye mchezo," Nabi alisema.

Yanga itaifuata KMC katika mechi ya raundi ya tatu itakayochezwa Oktoba 19, mwaka huu kwenye Uwanja wa Majimaji, Songea mkoani Ruvuma.

# STARS YAAHIDI KUIMALIZA BENIN

## ●●● Kocha atamba wako tayari kuendeleza ubabe, huku NBC ikimwaga...

**Na Saada Akida**

TUKO tayari! Hayo ni maneno ya Kocha Mkuu wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), Kim Poulsen kuelekea mchezo wa kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Dunia dhidi ya Benin utakaochezwa leo kwenye Uwanja wa Benjamini Mkapa jijini Dar es Salaam.

Stars itashuka uwanjani leo ikiwa na kumbukumbu ya kushinda mechi yake iliyopita dhidi ya Madagascar na kufikisha pointi nne, ambazo zimewaweka kileleni katika Kundi J ikifuatiwa Benin yenye pointi tatu, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) yenye pointi mbili na Madagascar wakishika mkia katika kundi hilo.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Poulsen alisema timu yake imejipanga vizuri kama ilivyo katika mchezo wao uliopita waliocheza hapa nyumbani dhidi ya Madagascar na wataingia uwanjani kutafuta pointi tatu muhimu.

Poulsen alisema anatambua mechi hiyo itakuwa ngumu kwa sababu asilimia 90 ya wachezaji wa Benin wanacheza soka la kulipwa Ulaya tofauti na Taifa Stars lakini ana imani na kikosi chake kimejipanga kupambana kusaka ushindi wa pili wakiwa nyumbani.

"Tumeingia kambini siku chache zilizopita ila tunafanya mazoezi vizuri, tuna matarajio makubwa ya kushinda mchezo huu, hayo ndio malengo yetu makubwa na hata Watanzania wote kwa ujumla," alisema Poulsen.

Naye Nahodha wa Stars, John Bocco alisema wamejiandaa vizuri na wanawataka mashabiki kujitokeza kwa wingi ili kuwasapoti kwa sababu malengo yao makubwa ni kushinda mechi zote za nyumbani ikiwamo dhidi ya Benin itakayochezwa leo.

"Tunatambua mechi itakuwa ngumu kwa kuwa hata wenzetu wamejipanga, lakini malengo yetu ni kuhakikisha tushinda mechi zote hasa za nyumbani ili kupambana na hatimaye kufuzu Kombe la Dunia mwakani," alisema Bocco.

Kwa upande wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Ofisa Habari na Mawasiliano, Clifford Ndimbo, alisema wamepokea barua kutoka FIFA ambayo inaruhusu mashabiki 10,000 kuingia uwanjani na kushuhudia mchezo huo.

Ndimbo alitaja kiingilio cha juu katika mechi hiyo ni Sh. 5,000 kwa mashabiki watakaokaa eneo la VIP B na eneo la mzunguko litakuwa ni Sh. 3,000.

Wakati huo huo, TFF imeingia mkataba wa miaka mitatu na Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) kwa ajili ya kuwa mdhamini mkuu wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Rais wa TFF, Wallace Karia alisema jana makubaliano hayo yanaanza rasmi msimu huu wa 2021/22 kwa kutoa kiasi cha Sh. bilioni 2.5 na sasa ligi hiyo rasmi itaitwa NBC Premier League.

Karia alisema TFF itafanya mazungumzo mengine na benki hiyo kwa ajili ya kukubaliana kiasi cha fedha kitakachotolewa kwa ajili ya misimu itakayofuata na lengo ni kuboresha na kuipandisha viwango ligi hiyo ambayo kwa sasa inashika nafasi ya nane Afrika. "Huu ni mkataba mnono katika udhamini wa ligi hiyo kwa msimu huu ambao haujawahi kutokea, huu ni mpango mkakati wangu ambao niliwahi kuahidi wakati naomba ridhaa ya kuongoza TFF. Awali alipoingia mdhamini klabu zilikuwa zikipata Sh. milioni saba, sasa hivi wadhamini wameongezeka na kila timu inapata zaidi ya Sh. milioni 500 ukijumlisha na fedha hizi za NBC," alisema Karia.

"Mbali na mdhamini huyo pia tunatarajia wiki ijayo kuingia mkataba na mdhamini mwingine wa ligi yetu, fedha zote ni mali ya klabu zinazoshiriki ligi hiyo na kugawiwa fedha zao kwa utaratibu maalum uliowekwa," alisema rais huyo.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa NBC, Theobald Sabi, alisema kuna mambo mengi yamewashawishi kuingia katika udhamini huo ikiwamo ubora ambao umefikiwa katika Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Tumefuatilia na kuona mpira wa miguu Tanzania unafuatiliwa sana na zaidi ya watu wasiopungua milioni 40, ni mchezo unaopendwa, tumeshawishika kujikita katika uwekezaji na udhamini mkuu wa ligi hii," alisema Sabi.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >